Jumanne Aprili 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581641

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



MO, BENCHIKHA KUJIFUNGIA SIMBA UKURASA 24

# Makonda aanza na maagizo sita

• **Magari** 100 yampokea, akijivunia alikotoka ameacha rekodi... *Uk. 2*



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda (katikati), akizungumza na umati wa wakazi wa Jiji la Arusha, waliofika kumpokea nje ya ofisi za mkuu wa mkoa huo, jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

UKURASA 2

**V8** lenye namba za serikali lanaswa likiwa limebeba wahamiaji haramu



UKURASA 3

**Mbunge** aibua madai mazito kinachoendelea Ngorongoro



UKURASA 5

**Udhibiti** ubora wa chakula kurudishwa TMDA baada ya kuhamishiwa TBS

## Wabunge walia sheria kikokotoo ifumuliwe tena

UKURASA 20



## ACT yataka Majaliwa akaone uhalisia Rufiji

UKURASA 20

**MICHEZO** GAMONDI AIONYA YANGA FA CUP UK.24

**KATUNI** UK.6

# Makonda aanza na maagizo sita

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, jana alikabidhiwa rasmi ofisi na aliyekuwa Mkuu wa mkoa huo, John Mongela na kuahidi kuanza na mambo sita atakayoanza nayo kazi.

Vile vile, alitoa miezi mitatu kwa Idara ya Ardhi, Ofisa wa Mipango miji kuondolewa na kuagiza watumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kufuatilia madai ya rushwa badala ya kuwasubiri viongozi wa siasa kuwaagiza kuchunguza.

Alisema ana mambo sita ya harakaharaka ambayo anaamini yapo katika ilani na serikali ni kuweka msingi wa haki.

"Nitakuwa kiongozi wa kutenda haki sitajitendea haki mimi mwenyewe na uzao wangu bali wananchi wanaodhulumiwa, kunyanyaswa, kucheleweshewa haki zao mimi nimekuja kusimama kwa niaba yao. Kama kuna mtu yupo Ngaramtoni ama kokote, ili mradi una haki yako na unajua ni haki yako sitaangalia kama hujasoma ama hauna hela, ndugu mwenye mamlaka nitasimama katika nafasi yangu kutetea haki yenu."

"Mmenifurahia sana ila tutageukana muda si mrefu, sitajali wewe ni nani, baba yako ni nani, ulipataje hicho cheo ama ulihonga kupata hiyo nafasi, sasa kama mnasema huyu alikuwa Mwenezi ametoka atakuja amepoa kuna watu wanasema sasa hivi atakuwa amejifunza, hakuna nilichojifunza zaidi ya kuwashughulikia wazembe, wavivu na wala rushwa sina elimu yoyote mimi, hata niwe mkuu wa mkoa wa siku moja inatosha, lakini awepo mtu mmoja ambaye anajua kuna mwanaume alipita hapa," alisema.

Aidha, alisema jambo la tatu ni ulinzi na usalama na ataendelea kukazia kuhakikisha Arusha inakuwa salama wanapatikana watalii wengi haitakuwa vizuri wasikie mkoa haupo salama. Pia, mji unatakiwa kuwa msafi na wenye nyumba wanatakiwa kupaka rangi ili upendeze.

**UTALII**

"Jambo la nne ni la utalii na Rais Samia Suluhu Hassan, alisema tutalivalia njuga kweli kweli. Utalii wetu upo katika maeneo matatu tuwe na utalii wa mikutano, nilikuwa nacheki idadi ya watalii hapa mkoani wana idadi yao na TTB na wenyewe wana idadi yao, hizi idadi hazioani maana yake kuna shida mahala."

Aliahidi kupita katika wilaya zote sita na kuwasikiliza wananchi kero zao na baada ya kuzichukua watakaa na chama na kuweka vipaumbele vya msingi kwa ajili ya kujibu haja za wannachi kwa mujibu wa maelekezo ya ilani.

Alisema anahitaji ushirikiano wao wanataka kutumikiwa kwa namna gani, bahati aliyokuwa nayo anaweza kuwa kiongozi wa aina yoyote ni kitu pekee ambacho anamshukuru Mungu.

Alisema wakitaka Arusha ibadilike uwe mji wenye amani na utulivu, mwananchi anaweza kusahau mahala simu yake na kuikuta, uwe mji wa kibiashara watu hawafungi maduka saa 11 jioni wanakesha kama ilivyo Kariakoo na barabara zipitike kwa lami, inawezekana.

"Chochote mtakachokitaka kitakuwa kwa sababu kubwa mbili kwa kumtanguliza Mungu na jambo la pili ni kwa kuwa Rais Samia anaipenda Arusha mpaka akamtoa mwanawe kwenye Uenezi na kumleta Arusha kuwa mkuu wa mkoa, huo ni upendo wa namna gani jamani," aliwahoji wananchi.

Aidha, alisema wanataka kujenga demokrasia ya kweli, uhuru wa kuandamana na siku nyingine wamualike katika hayo maandamano na atashiriki nao vizuri.

Kiongozi huyo alisema kuwa bila maombi asingekuwapo, kwa kuwa katika ziara zake za uenezi amekoswa mara tatu kupoteza maisha na kwamba anawashukuru viongozi wote wa dini wanaoendelea kumwombea.

"Eneo linalonuka rushwa katika nchi hii ni kwenye ardhi, kama hapa Arusha tunaacha mipango miji tumezalisha ujenzi holela, kuna rushwa pale...hatuna 'plan' halafu kuna mtu anaitwa ofisa mipango miji..."

"Haiwezekani akaendelea kukaa hapa mji wa kitalii tunajenga holela, hatumhitaji mtu wa aina hiyo akija ofisini utasikia hivi viwanja ni 'potential' msije kuhangaika kunitafutia kiwanja, hangaika kuwahudumia wananchi."

Alisema hata watalii wanapofika wanashangaa mji wa kitalii hakuna mipango miji na kuwatumia salamu watu wa ardhi kuwa kama hawasimamii upangaji mji, atawapangia.

Aliagiza pia ndani ya miezi mitatu apatiwe ripoti ya migogoro ya ardhi iliyotatuliwa na mazingira yaliyowekwa kutojitokeza tena kwa migogoro hiyo.



Aidha, alisema hataki kusikia anaielekeza TAKUKURU kuchunguza rushwa kwa kuwa ni wajibu wao na endapo hilo likijitokeza, atawasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, amuondoe mtumishi wake.

Alisema yeye ni Mwenezi aliyevunja rekodi kukaa katika kipindi kifupi (siku 162) kwenye historia, lakini hakuna Mwenezi aliyekaa miezi mitano na kutembea kilometa 11,593, mikoa 23 na kufanya mambo makubwa ambayo hayawezi kufutika kama alivyofanya yeye.

"Sio muda gani uliokaa, bali umeacha alama gani, kwa hiyo hata hapa sitaangalia muda, hapa naona kama nimechelewa kuanza kazi huu muda nilitakiwa niwe 'site' nina kiu ya kuwatumikia wananchi," alisisitiza.

Awali, katika mapokezi yake Makonda aliwasili Uwanja wa Ndege Arusha (Kisongo), majira ya saa 4:30 asubuhi kwa ndege ya Shirika la Precision Air 5H-PWE.

Msafara wake kuelekea ofisi za makao makuu ya mkoa huo, uliongozwa na magari zaidi ya 100 baadhi yakiwa ya kifahari.

Waendesha bodaboda na bajaji walipamba msafara huo huku mamia ya wananchi wakiwa wamesimama pembezoni mwa barabara kutoa uwanja wa ndege kueleka Arusha mjini wakimpungia kwa ishara ya kumkaribisha kwenye mkoa huo.

Kiongozi huyo hakupanda gari la serikali bali alitumia moja ya gari yanayotumika kubeba watalii kwenye msafara huo lenye namba za usajili T625 EDP, akiwapungia mkono wananchi akiwa na familia yake mke na mtoto wake.

Akiwa katikati ya Jiji la Arusha, alipita barabara ya Soko Kuu la Arusha na wafanyabiashara walisimamisha shughuli zao kwa muda kumlaki huku msafara wake ukisababisha msongamano wa magari ndani ya jiji hilo baada ya vyombo vingine vya usafiri kusimamishwa kwa muda.

Akiwa jijini humo, alipita barabara ya stendi kuu ya mabasi Arusha na baadaye kuelekea katika ofisi za Mkoa wa Arusha kwa ajili ya utaratibu wa makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Mkuu wa Mkao wa Arusha, John Mongela, ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara.

Makonda alifika ofisini saa 5:30 asubuhi akisubiriwa kwa shauku na wananchi eneo la kiwanja ofisi pamoja na viongozi wa chama na serikali kutoka ngazi mbalimbali.

**MONGELA**

Mongela alisema Makonda ni ndugu yake na mafanikio atakayoyaleta Arusha yatamgusa moja kwa moja na yupo tayari kumpatia ushirikiano kwa kila jambo.

"Makonda ni mstaarabu, muungwana, lakini ukweli ni kwamba akisema leo anataka litokee, ndugu zangu msije kusema mbona Mongela alikuwa anatubembeleza, hapana nafikiri sasa ni muda wa mkoa kukimbia tumpe ushirikiano wa kutosha haya ni maendeleo yetu sote," alisema Mongela.

Alikumbusha kuwa mwaka huu kuna uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwataka wananchi wakiunge mkono Chama Cha Mapinduzi ili kukamilisha maendeleo zaidi anachokiahidi watendaji siasa za kistaarabu za kiungwana na kukifanya chama kupata ushindi.

## Shangingi la serikali lakamatwa likiwa na wahamiaji haramu 17

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JESHI la Polisi mkoani Manyara limekamata shangingi lililopachikwa namba za usajili wa serikali, VXR V8 likisafirisha wahamiaji haramu 17 raia wa Ethiopia.

Shangingi hilo limenaswa likitumia namba za usajili STL 1964, limebainika kuwa na namba nyingine T 723 BSF. Lilikamatwa juzi Aprili 7 katika Kijiji cha Kiongozi, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara.

Machi 23, mwaka huu, gari lingine aina ya Toyota Land Cruiser VXR V8 lililokuwa linapeperusha bendera ya CCM, nalo lilikamatwa likiwa na wahamiaji haramu 20 raia wa Ethiopia katika kizuizi cha Minjingu, wilayani Babati.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Lucas Mwakatundu, raia hao wa Ethiopia waliokamatwa wakisafirishwa kwa gari la umma, wanakabiliwa na kosa la kuingia nchini bila kufuata taratibu na kutokuwa na vibali.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mwakatundu alisema raia hao wa Ethiopia wamekamatwa katika Kijiji cha Kiongozi, wilayani Babati, wakisafirishwa kwenda Afrika ya Kusini kwa ajili ya kutafuta ajira na makazi.

Kamanda Mwakatundu alisema mpaka sasa hawajabaini mmiliki halisi wa gari hilo lililokuwa na namba mbili tofauti; wanaendelea na uchunguzi kubaini mmiliki halali.

Alisema kuwa raia 17 wa Ethiopia walikamatwa wakiwa ndani ya gari hilo ambalo wahusika waling'oa baadhi ya viti ili waweze kuenea wote.

"Tunatarajia kuwakabidhi Jeshi la Uhamiaji rai hao 17 wa Ethiopia 17 kwa hatua nyingine ikiwamo kufikishwa mahakamani na kujibu mashtaka yanayowakabili," alisema Mwakatundu.

**Alisema kuwa raia 17 wa Ethiopia walikamatwa wakiwa ndani ya gari hilo ambalo wahusika waling'oa baadhi ya viti ili waweze kuenea wote.**


**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KASULU**
**MAHALI: KASULU**
**MAOMBI NA 9 MWAKA 2023**
**EDWARD NDIMUGWANKO MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KASUKILO KASHIKA MITILA MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA: KASUKILO KASHIKA MITILA**

**POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 15 mwezi 5 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mheshimiwa MOURICE mwenyekiti wa Baraza Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 mwezi 3 mwaka 2024

MWENYEKITI



**KUPOTEA KWA CHETI**



**HOSIANA RICHARD SAWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1898-0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TUMAINI NKEREZANGE SEKONDARI** mwaka **2012**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control number: **9910840746747.**



**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**MIRATHI Na. 629 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**WILLIAM ESTOMICH URUNO**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**HELLEN WILLIAM URUNO**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 Mwezi wa 04, 2024.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 28 Mwezi wa 03, 2024.

NAIBU MSAJILI

HABARI KITAIFA

# Mbunge aibua madai mazito kinachoendelea Ngorongoro

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Ngorongoro, Emmanuel Ole Shangai ameitaka serikali kuja na kauli moja inayotaka wakazi wote wa eneo la Ngorongoro kuondoka kwa lazima kuliko kuendelea kufanya alichokiita kuwawekea vikwazo katika huduma muhimu za kijamii, ikiwamo upatikanaji maji safi na salama.

Shangai alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akichangia mapatio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuwa kwa sasa hali ya wakazi wa eneo la Ngorongoro imeendelea kuwa ngumu kutokana na vikwazo wanavyowekewa.

Mbunge huyo alisema serikali inatakiwa itoe tamko kwa wananchi zaidi ya 108,000 walioamua kubaki katika Tarafa ya Ngorongoro baada ya wale wengine 7,000 kuhamia Msovera na wao watoke kwa lazima kwa kuwa huduma nyingi zimefungwa kwa sasa.

Alitaja huduma zilizofungwa kwa wananchi hao kuwa ni pamoja na zaidi ya shule 27 za msingi katika tarafa hiyo ambazo aliliambia Bunge kuwa zote zimezuwa kujenga wala kukarabati vyoo, hali inayosababisha walimu na wanafunzi kujisaidia porini.



Mbunge huyo pia alisema kuna shule ya msingi ya bweni imesitishiwa huduma ya maji, hali inayowalazimu wananchi kufuata huduma ya maji mtoni na kuhatarisha maisha yao.

"Kwanini tunafanya hivi? Kila mwananchi ana haki ya kupata huduma na zoezi la kuhama lilikuwa la hiari na Waziri Mkuu alipozungumza na wananchi alithibitisha hilo. Iweje sasa tuanze kuwawekea vikwazo vya maendeleo?" Shangai alihoji.

Alisema ni zaidi ya miaka mitatu sasa wananchi hawapati huduma stahiki zikiwamo huduma za afya ambazo zimekuwa hafifu na kuhoji wananchi wameikosea nini serikali kwa kuwa wako katika eneo hilo kisheria. Mbunge huyo alisema licha ya jimbo kupata maendeleo mbalimbali ikiwamo kujengwa shule za sekondari na msingi kutokana na jiografia ya mazingira ya wanyama katika shule hizo, wanafunzi hawatafaidi kutokana kutokuwa na mabweni pamoja na nyumba za walimu ili wanafunzi wapate huduma ipasavyo.

"Wakati wa hotuba ya kuhitimisha hoja hii, mniambie kwamba serikali ina mpango gani na wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro?

Isitoshe kwenye geti la Ngorongoro wananchi wakirudi jioni hawaruhusiwi kuingia mpaka wawe na vitambulisho vya wapigakura ilhali wapo baadhi ya vijana wenye umri wa chini ambao wanawalazimisha kwenda polisi kuchukua taarifa inayowatambulisha," alisema.

Mbunge Shangai pia alisema hata wafanyabiashara wa mifugo wanazuiwa kufanya shughuli zao, wakitakiwa kubeba ng'ombe kwa malori ilhali hakuna miundombinu ya barabara ya kupitisha magari hayo.

"Kama imefika wakati ni bora tuwaambie kwamba hawahitajiki katika eneo hilo ili waondoke kuliko kuendelea kuwapa mateso maana upo pia mradi wa elimu wa wanafunzi kusomeshwa vyuo vikuu na vyuo vya kati, lakini wanafunzi zaidi ya 154 waliopitishwa na Baraza la Wafugaji wamesitishiwa ufadhili hali inayosababisha ongezeko la watoto wa kike kujihusisha na vitendo vibaya vya kujiuza ili kupata chochote," alisema.

Vilevile, alisema wafanyabiashara wameanza kugomea minada baada ya serikali kupitia halmashauri kuongeza kodi katika mifugo ambapo kwa mbuzi imeongezeka kutoka Sh. 2,500 hadi 8,000 huku madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri wakiwa hawajui na ushuru huo unakusanywa kwa kutumia wanajeshi.

Katika hotuba yake bungeni wiki iliyopita wakati wa kuwasilisha hoja hiyo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema kuwa atika jitihada za kulinda bioanuai ya hifadhi na kuboresha maisha ya wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, serikali imeendelea kuwahamisha kwa hiari wananchi kutoka ndani ya eneo la hifadhi kwenda katika maeneo yaliyotengwa na serikali huko Msomero wilayani Handeni, Saunyi (Kilindi), Kitwai (Simanjiro) na maeneo mengine ambayo wananchi wamechagua.

Waziri Mkuu alisema kuwa katika awamu ya pili, jumla ya nyumba 5,000 zinajengwa katika maeneo ya Msomera (2,500), Saunyi (1,000) na Kitwai (1,500) ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi 21 Februari 2024, jumla ya nyumba 700 zimekamilika na nyumba 1,800 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

"Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Februari 2024, jumla ya kaya 491 zenye watu 3,451 na mifugo 14,599, zimehama kwa hiari na hivyo kufanya jumla ya kaya zilizohamia tangu kuanza kwa zoezi hili Julai 2022 kufikia 1,042, ikijumuisha jumla ya watu 6,461 na mifugo 29,919," Majaliwa alifafanua.


Nipashe MWANGA WA JAMII
The Guardian www.ippmedia.com

**Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited**



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia wikiendi ijayo ya tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya Nipashe na The Guardian yatakuwa yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI HUDUMA YA : UHAKIKI WA UFANISI, MAJARIBIO NA UZINDUZI WA MITAMBO YA EACOP KUMBUKUMBU NA. REQ-00000458**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kusaidia kutoa Huduma ya uhakiki wa Ufanisi, majaribio na uzinduzi wa mitambo ya EACOP kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania bomba litakatisha miko minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga,tawala za Halmashauri 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

UHAKIKI WA MITAMBO NA VIFAA VYA UMEME KAMA VINAFANYA KAZI IPASAVYO
- Kufanya shughuli za Uhakiki wa ufanisi, majaribio na Uzinduzi wa E&I (Majaribio ya ufanisi, Majaribio ya program, Majaribio ya kiutendaji).
- Kutoa rasilimali kwa ajili ya kuendesha chumba cha ufundi (LOTO, utatuzi wa matatizo ya kiufundi).
- Kutoa usaidizi kwa wazabuni wakati wa uhakiki, majaribio na uzinduzi.

UHAKIKI WA UFANISI WA VIFAA VYA MAWASILIANO
- Kufanya shughuli za Uhakiki wa Ufanisi wa vifaa vya mawasiliano (Majaribio ya ufanisi, Majaribio ya programu, Majaribio ya kiutendaji).
- Kutoa rasilimali kwa ajili ya kuendesha mfumo wa mawasiliano mpaka pale utakapokabidhiwa kwa EACOP FOPS (LOTO, utatuzi wa matatizo ya kiufundi).

UHAKIKI NA MAJARIBIO YA UFANISI WA MITAMBO NA MABOMBA YA MRADI WA EACOP
- Kufanya shughuli za Uhakiki wa Ufanisi wa mitambo na mabomba (Uandaaji wa vifaa vya mitambo, Majaribio ya ufanisi, Majaribio ya programu).
- Kutoa rasilimali kwa ajili ya kuwezesha uandaaji wa mitambo na mabomba ili kuwezesha majaribio ya kiutendaji (kutembelea eneo la kazi, uwekaji wa mifumo, utunzaji na usafirshaji wa vifaa vya mitambo nk).
- Usaidizi na Msaada wakati wa majaribio ya kuvuja kwa Nitrojen.

HUDUMA YA MANUNUZI
- Kutoa huduma ya Manunuzi wakati wowote inapohitajika ili kukamilisha uhakiki wa ufanisi, majaribio na uzinduzi (kazi mahususi, vipuri, na vifaa vya matumizi, n.k.)

**VIGEZO MUHIMU:**

Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu, na uwezo wa kutoa huduma katika wigo husika.
- Maelezo ya miradi au shughuli zinazofanana zilizokwishafanywa zinazotoa uthibitisho wa timu iliyopo yenye weledi, ufahamu wa maeneo ya bomba, na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA na usajili unaopatikana BRELA (ambatanisha kivuli cha cheti). Uthibitisho wa usajili toka UWURA.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani ni Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.
- Uzoefu wa katika shughuli za uhakiki wa ufanisi na majaribio ya miundombinu ya Mafuta na gesi.

Kampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **8 Mwezi May 2024** jioni saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000458** - Uhakiki wa Ufanisi, Majaribio na Uzinduzi wa Mitambo ya EACOP. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Serikali yaandaa taarifa hali ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI inatarajia kutoa taarifa ya mazingira Juni mwaka huu itakayoonesha hali ya mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mwera (CCM), Zahor Mohammed Haji.

Mbunge huyo alihoji, "pamoja na serikali kutoa elimu, imefanya tathmini kuona elimu wanayoitoa imewafikia wananchi?"

Dk. Jafo, akijibu swali hilo, alisema taarifa hiyo itaonesha hali ilivyo siku ya mazingira duniani.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji sababu za serikali kutoelimishi wananchi kujiepusha na madhara yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi hadi pale maafa yanapotokea.

Akijibu swali hilo, Dk. Jafo alisema serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kwa kuelimisha wananchi kuhusu madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi ili wajilinde na maafa yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alitaja baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kupitia njia mbalimbali hasa vyombo vya habari na mitandao ya kijamii inayolenga kukuza uelewa kwa makundi mbalimbali katika jamii hasa wakulima, wavuvi na wafugaji kuhusu mbinu bora za kilimo, ufugaji na uvuvi endelevu zinazoweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, pia kujilinda dhidi ya maafa yanayoweza kutokea kwa jamii.

"Na kwa kutambua umuhimu huo, serikali kuanzia mwaka 2023 na kuendelea kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru imekuwa na ujumbe mahususi wa kuhifadhi mazingira ili kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chaya alitaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kunusuru wananchi wa kata ya Sanza kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha Bwawa la Sanza kuchepuka na kuingia kwenye makazi yao.

Waziri Jafo, akijibu swali hilo, alikiri kuwa na taarifa hiyo na kwamba ni maeneo mengi yamekumbwa na hali hiyo kwa kiasi kikubwa ikiwamo Mpwapwa, Mvomero na Manyoni.

# Watengeneza mashine ya kutibu ugonjwa wa manjano

**Na Maulid Mmbaga**

WAHANDISI na wataalamu wa masuala ya afya kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya Doris Mollel Foundation wametengeneza mashine ya kisasa inayotumika kutibu watoto wachanga wanaozaliwa na tatizo la ugonjwa wa manjano.

Mkurugenzi Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Doris Mollel alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kimataifa wa afya ya wanawake, uliohudhuriwa na wajumbe zaidi ya 800 kutoka mataifa 41 duniani.

Mkutano huo ulifanyika kuanzia Aprili 6 mwaka huu hadi jana, ukiwa na lengo la kujadili changamoto, mafanikio na hatua za kuchukua kuimarisha uongozi kwa wanawake katika sekta ya afya duniani.

Kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Tanzania imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto kutoka 67 hadi 43 katika kila vizazi hai 1,000, lakini anakiri bado wanakabiliwa na changamoto katika kupunguza vifo vya watoto wachanga.

"Hili ndilo jambo kubwa kama sekta ya afya ambalo tunakwenda kuhangaika nalo katika kuboresha huduma lakini pia kuhakikisha tunapunguza changamoto hiyo kutoka kwa watoto wenye umri wa siku sifuri hadi 28," alisema Ummy.

Doris alisema kazi kubwa wanayoifanya ni kuhakikisha wanaisaidia serikali kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati na wale wanaopatwa na maradhi mbalimbali, na kwamba wanaendelea kutengeneza vifaa tiba vitakavyosaidia kutatua matatizo yanayowakumba watoto.

"Moja ya vifaa ambavyo tumevileta hapa ni kifaa ambacho kinaweza kusaidia mtoto ambaye amepata changamoto ya kuugua ugonjwa wa manjano, ni tatizo linaloweza kumharibu mtoto hata ubongo pamoja na ukuaji wake kwa ujumla," alisema Doris.

Aliongeza kuwa pia wanasaidia watoa huduma ya afya kupata vifaa tiba ambavyo vinaweza kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.

Hata hivyo, Doris alisema changamoto inayowakabili katika sekta ya afya ni kupata wanawake wengi ambao wanaaminika katika utendaji.

"Wito wangu tunatamani kuona viongozi wengi wa kike wananyanyuka kutoka sekta ya afya, tulionao bado hawatutoshi, tunahitaji hamasa zaidi, ili waweze kunyanyua sekta hii kwa ukubwa wake, kutengenezwe programu ambazo zitawanoa madaktari wetu wa kike waweze kumudu majukumu makubwa," alisema Doris.

HABARI KITAIFA

# ZECO sasa kusambaza nguzo za zege Zanzibar

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imesema ipo haja Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuanza mchakato wa kuhama kutoka matumizi ya nguzo za umeme za miti hadi kutumia nguzo za zege, ili kuokoa gharama kubwa inayotumika kubadilisha miundombinu hiyo.

Kamati hiyo ilielekeza hayo juzi ilipofanya ziara maalum kwenye kiwanda cha kuzalisha nguzo za umeme za zege kinanachomilikiwa na Kampuni ya Derm Group kilichoko Bagamoyo, mkoani Pwani.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanaasha Khamis Juma, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa inatumia gharama kubwa kwa kufanya maboresho ya mara kwa mara ya nguzo za umeme za miti ambazo huharibika kwa sababu mbalimbali, ikiwamo mvua kubwa, upepo, kuungua au kushambuliwa na wadudu.

"Katika ziara yetu kwenye kiwanda hiki, tumeona wana teknolojia nzuri ya kuzalisha nguzo za zege na ni imara sana ambazo siyo rahisi kuharibika.

"Sisi kama kamati tumeona kwamba SMZ kuna haja zitoke kwenye matumizi ya nguzo za miti na kuhamia kwenye hizi za zege kwa sababu ukiweka hizi hazihar-ibiki.

"Tumeambiwa TANESCO wenyewe tayari wameshaanza, tunalishauri na ZECO wafanye hivyo kwa sababu huenda hii ikawa suluhisho la tatizo la kukatika umeme na wananchi wakawa na umeme wa uhakika na kuzalisha zaidi," alisema.

Mjumbe wa kamati hiyo, Asha Abdallah Mussa, alisema matumizi ya nguzo hizo za umeme za zege yatasaidia pia kwenye utunzaji mazingira na kupunguza ukataji miti.

"Na tumeona kwamba nguzo hizi za umeme za zege zinadumu kwa muda mrefu kuliko za miti. Kwahiyo, kwa sasa ZECO ione umuhimu wa kuhama kutoka huko," alisema Asha.

Mwakilishi kutoka ZECO, Shariff Sheikh Robart, alisema kupitia ziara hiyo, wameamua kuingia mkataba wa kupatiwa nguzo za umeme za zege 380 ambazo wataanza nazo kwa hatua za awali.

"Tumejifunza mengi katika ziara hii na kubwa zaidi tumeona tunaweza kuondokana na matumizi ya nguzo za miti na kuingia katika matumizi ya nguzo za zege kwa sababu tumeona hata bei yake haitofautiani sana na ile ya nguzo za miti, changamoto tunazozipata kutokana na matumizi ya nguzo hizi za miti za umeme ni nyingi na mojawapo ni marekebisho ya mara kwa mara.

"Pamoja na kwamba tumekuwa tukiziwekea dawa ili zisiharibike, lakini zimekuwa hazichukui muda mrefu zinaliwa na wadudu na mwisho wa siku tunalazimika kuzibadilisha, tunapata hasara nyingi kutokana na matumizi ya nguzo hizi za miti," alisema.

Mkurugenzi wa Derm Group ambao ndio wazalishaji wa nguzo hizo za umeme za zege, Bridget Temba, alisema nguzo hizo zina uwezo wa kudumu kwa zaidi ya miaka 100 tofauti na za mbao.

"Hizi zenyewe hata kama itanyesha mvua kubwa au kutokea moto, haziharibiki, kwa hiyo ukiziweka unakuwa na uhakika, hutatumia gharama nyingine kwa ajili ya matengenezo,"alisema Bridget.

## Udhibiti ubora wa chakula mbioni kurejeshwa TMDA

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imesema suala la kurejesha usimamizi na udhibiti ubora wa chakula na vipodozi kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) linaendelea kujadiliwa ndani ya serikali na likikamilika, mapendekezo ya utekelezaji yatawasilishwa bungeni.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo.

Mbunge huyo alihoji mpango wa kurejesha kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) suala hilo kwa kuwa imeacha masuala ya chakula na inakinzana na utaratibu wa usimamizi wa chakula na dawa duniani.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali katika kuimarisha mazingira ya biashara nchini, ilifanya uamuzi kupitia Bunge kuhamisha majukumu ya usimamizi na udhibiti ubora wa chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa TFDA na kuyapeleka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambako ndiko afua zote za usimamizi zinatekelezwa kwa sasa.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema TBS imeonekana kushindwa kusimamia masuala ya chakula na Kamati ya Bunge ya Afya imeshauri masuala hayo yarejeshwe TMDA lakini kuna kamati zingine zimeshauri TFDA irudi.

Alihoji sababu za mchakato huo wa serikali kutofanyika haraka ili kuimarisha masuala ya usimamizi wa chakula.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mollel alisema serikali itaendelea na mchakato huo kama ilivyofanyika awali na itakapokamilisha, watawasilisha bungeni kama ilivyoshauriwa na Kamati ya Bunge.

## ETG yatoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalumu

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Kimataifa inayofanya shughuli mbalimbali katika sekta ikijumuisha Usafirishaji na uagizaji bidhaa za kilimo imetoa msaada fedha  na vitu mbalimbali katika kituo cha watoto yatima cha Hisani kilichopo Kibada Kigamboni .

Msaada uliotolewa na Kampuni hiyo ni pamoja na magodoro, friji, Mchele, Unga, mafuta ya kupikia, sukari, Korosho, maharage,maziwa,mikate, biskuti, juisi, mikate na matunda.

Akizungumza wakati akitoa msaada huo Mkuu wa Kampuni ya ETG Tanzania, Niladdri Chowdhury alisema wameamua kutoa msaada huo kama Sehemu ya uwajibikaji wao katika jamii.

"Tumepata heshima kubwa ya kutembele kituo cha watoto yatima cha Hisani katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan kutoa misaada mbalimbali "alisema

Nakuongeza kuwa"
Ni bahati kwetu na inatia moyo na kupata ufahamu wa kina juu ya maisha ya watoto ambao wanakabiliwa na chagamoto mbalimbali katika umri mdogo"aliongeza Chowdhury

Aidha alisema wanatumaini kuwa kupitia msaada walioutoa katika kituo hicho utaleta mabadiliko .

Kwa upande wake Mwanzilishi wa Kituo hicho, Hidaya Mtalemwa aliiushukuru uongozi mzima wa ETG kwa msaada wa vitu mbalimbali.

Alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 2010 kwa lengo la kusaidia watoto wasiojiweza ili wapate maradhi staiki .




*Mkurugenzi wa Makampuni ya ETG Tanzania, Niladdri Chowdhury ( kushoto), akimkabidhi msaada wa fedha taslimu na vitu mbalimbali vikiwepo magodoro kama msaada kwa watoto wanaolelewa kwenye kituo maalumu Kulia ni Mwanzilishi wa kituo cha hisani Hidaya Mtalemwa*

Hata hivyo alisema kituo hicho kinakabiliwa na chagamoto mbalimbali ikiwemo kutokuwa na Makazi ya kudumu.

Hidaya aliziomba Kampuni na Taasisi mbalimbali ikiwemo wadau, Serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma na kuwasaidia .

"Watoto hawa wakipata mahitaji mazuri ikiwemo elimu bora, maradhi, hii itasaidia kuondokana na chagamoto ya kuama kila wakati kwa ajili kutafuta sehemu ya kuishi "alisema Hidaya

Aliongeza kuwa kituo hicho kinajumla ya watoto 82 ambapo 50 ni wakike huku wakiume wakiwa 32.

Aidha alitoa wito kwa wadau wengine kuinga mfano wa Kampuni ya EGT wa kuwatembelea watoto yatima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyoo vya shule kujaa ni hatari kwa wanafunzi

**KATIKA** toleo letu la jana tuliripoti taarifa kuhusu wazazi wa Shule ya Msingi Tembo mjini Songea kutishia kutorudisha wanafunzi shuleni kutokana na vyoo kujaa.

Shule hiyo yenye matundu 10 ya choo, inaelezwa kujaa na kwamba wanafunzi wanalazimika kwenda kujisaidia vichakani.

Walimu pia ambao wanategemea choo hicho nao wanalazimika kwenda vichakani kwenda kujihifadhi.

Kitendo cha kwenda kujisaidia vichakani ni hatari kwa wanafunzi hao kwa sababu wanaweza kukutana na wadudu wabaya na kuwadhuru.

Vile vile, ni hatari kwa afya kwa sababu wanaweza kuambukizana magonjwa ya mlipuko ukiwamo wa kipindupindu au ugonjwa wa matumbo.

Vyoo vya shule kujaa bila hatua kuchukuliwa kwa kuvinyonya ni uzembe ambao hauwezi kuachwa uendelee.

Wanafunzi pamoja na walimu wao wanatakiwa kuwa katika mazingira mazuri ya kusomea na kufundishia.

Mwanafunzi hawezi kuwa makini katika masomo kama atakuwa anataka kwenda kujisaidia halafu anakosa sehemu salama ya kwenda kujisitiri.

Kwa wanafunzi wa kike ni hatari zaidi kwa kuwa wanapokuwa kwenye siku zao za hedhi wanahitaji sehemu safi na salama ya kujihifadhi.

Mahudhurio ya wanafunzi shuleni yanaweza kuwa mabaya na kusababisha matokea ya mitihani kutokuwa mazuri kutokana na kushindwa kukosa baadhi ya masomo wanapokuwa kwenye hali ya kujitaji sehemu salama ya kujihifadhi.

Imeelezwa kuwa tangu choo cha shule hiyo kijae ni muda mrefu na viongozi karibu wote wa Manispaa ya Songea wana taarifa zake, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo pia anasema mazingira ya choo ni mabaya kwa sababu matundu yote 10 yameziba na kusababisha haja kubwa kusambaa.

Hii inahatarisha afya za wanafunzi kupata magonjwa ya mlipuko na kama hatua za haraka hazitachukuliwa italeta majangwa makubwa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo amezungumzia licha ya jitihada kuendelea kufanyika baina ya wazazi, uongozi wa shule na serikali kulimaliza tatizo hilo, utatuzi wake una suasua.

Walimu 17 wanaofundisha shule hiyo nao wanategemea kujisitiri kwenye matundu hayo 10 ya choo yanayotumiwa na wanafunzi wa jinsi zote.

Viongozi wa manispaa hiyo wanakiri kuwa hali ni mbaya katika shule hiyo huku wakisisitiza hatua zinachukuliwa.

Moja ya hatua hiyo ni halmashauri kutenga Shilingi milioni tano kwa ajili ya unenzi wa choo na vile vile kuhimiza wazazi wa wanafunzi wanaosoma shule hiyo kuona umuhimu wa kuchangia ujenzi huo.


Wazazi kwa upande wao toka mwanzo wameonyesha jitihada za kuhamasishana kuchangia ujenzi huo kwa sababu wanaoathirika ni watoto wao na wakipata madhara, gharama za kuwatibu zitakuwa kubwa.

Hata hivyo, baadhi ya wazazi hao wamedai kuwa pamoja na kufanikisha uchangiaji huo, fedha kidogo iliyopatikana ilielekezwa kwenye chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Fedha kuelekezwa kwenye chakula ni jambo zuri, lakini wanafunzi wakishakula watahitaji kwenda kujisaidia, je wataendelea kwenda vichakani?

Ni vyema zikachukuliwa hatua za haraka wakati ujenzi wa vyoo vingine ukisubiriwa, kujenga vyoo vya muda ili wanafunzi na walimu wao wapate kusitirika na kuepukana na majanga ya kwenda kujisaidia vichakani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Uhaba wataalamu maabara shuleni ungetafutiwa ufumbuzi wa kudumu

**MIAKA** ya nyuma, baadhi ya sekondari hasa za kata, hazikuwa na majengo wala vifaa vya maabara. Jitihada zikafanyika na bado zinaendelea kufanyika, lengo likiwa ni kila shule ya sekondari kuwa na maabara.

Serikali iliweka kazi katika ujenzi huo kwa kushirikisha wananchi waliochangia kwa hali na mali na wengine nguvukazi yao, ili shule hizo za umma ziweze kufundisha kwa vitendo masomo ya sayansi.

Hatua hizo zimechukuliwa, kutokana na ukweli kwamba maabara hizo zinamjenga mwanafunzi katika masomo ya sayansi kwa vitendo badala ya kufundishwa kwa nadharia na kushindwa kuelewa vizuri.

Kwa maana hiyo, kila sekondari inatakiwa kuwa na maabara tatu za masomo ya fizikia, kemia na baiolojia ili kufanikisha ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo.

Hadi sasa kwa juhudi hizo, majengo mengi ya maabara yatakuwa yamejengwa katika sekondari mbalimbali ingawa, pia kuna changamoto kadhaa ambazo zimekuwa zikilalamikiwa.

Miongoni mwa changamoto, ni kutokamilika kwa ujenzi wa majengo ya maabara au mengine kukamilika, lakini yanakaa muda mrefu bila kutumika kutokana na ukosefu wa vifaa vya maabara.

Changamoto nyingine inayotajwa na wadau wa elimu, ni baadhi ya sekondari kuwa na maabara, lakini zinakosa walimu wa masomo ya sayansi na wataalam wa maabara hizo (Laboratory Technicians).

Ukosefu huo wa wataalam wa maabara na walimu wa masomo ya sayansi, vinaweza kurudisha nyuma jitihada za mafunzo kwa vitendo, katika sekondari, licha ya kuwapo kwa maabara katika baadhi ya shule.

Pia, imekuwa ikielezwa kuwa kutokana na ukosefu huo wa wataalam wa maabara, baadhi ya walimu wa masomo ya sayansi ndio wanageuke kuwa wataalam wa maabara hizo.

Ninaamini, kwa kutumia walimu wa masomo ya sayansi, inaweza kuwa vigumu wanafunzi kufundishwa kukamilifu, kutokana na kwamba si wataalam wa kutumia maabara hizo.

**Kwa kuwa serikali ilishatangaza mwongozo mpya kuwa masomo ya sayansi ni lazima kusomwa na wanafunzi wote wanaosoma elimu ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.**

Utumiaji wa walimu hao inaweza kuwa mazuri, lakini sidhani kama wanaweza kuwafikia wataalam wa maabara hizo na kuwafanya wanafunzi wasipate kile wanakihitaji kujua maabara hizo.

Hivi karibuni, nilihudhuria semina moja jijini Dar es Salaam iliohusu masuala ya elimu, baadhi ya wanafunzi wakaibua hoja yaukosefu wa wataalam wa maabara katika baadhi ya sekondari.

Kwa mujibu wao ni kwamba, walimu wa masomo ya sayansi ndio wamegeuka kuwa wataalam wa maabara, kitendo ambacho wanaamini kuwa hakina msaada mkubwa wa kimasomo kwao.

Zinahitaji hatua za haraka ili kufanikisha azma ya kuwa na mafanikio kwenye elimu kwa vitendo, kwa kila shule kuwa na wataalam hao badala ya kutumia walimu au kutokuwa na wataalam hao kabisa.

Juhudi zilizotumika hadi kila sekondari ikawa na majengo ya maabara, zingetumika pia kuajiri wataalam hao ili wasaidie wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.

Ikumbukwe kuwa, kama ambavyo ukosefu wa maabara hizo umekuwa ukichangia wanafunzi wa masomo ya mkondo wa sayansi kutofanya vizuri katika mitihani yao, ndivyo inaweza kutokea wasifanye vizuri kutokana na ukosefu wa watalaam wa maabara.

Kwa kuwa serikali ilishatangaza mwongozo mpya kuwa masomo ya sayansi ni lazima kusomwa na wanafunzi wote wanaosoma elimu ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Ulazima huo pia ungekwenda sambamba na upatikanaji wa wataalam wa maabara kwa kila shule ili kusaidia kuwaandaa vyema wataalam wa baadaye wa fani mbalimbali nchini.

# Rais tusaidie kupata malipo ya mauzo ya vanila 1,057,603,400/-

**Ndugu mhariri;**

Umoja wa Wakulima wa Vanila Mkoa wa Kagera (AMCOS) tuliuza vanila tangu Julai mwaka jana, 2023 kwa kampuni ya SOSAKA ambayo ndiyo kampuni iliyoidhinishwa kununua vanila mkoani Kagera kwa wilaya zote za Bukoba Vijijini, Misenyi, Kyerwa, Muleba na Karagwe kwa kiasi cha Sh. 15,000 kwa kilo ya vanila mbichi.

Ndugu mhariri, kampuni haijatulipa wakulima fedha yote inayodaiwa. Tunaomba taarifa hii ifikishwe kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa barua ya wazi kupitia gazeti lako la Nipashe.

Hatua zilizochukuliwa na Umoja wa Wakulima wa Vanila (AMCOS) ambazo hazikuzaa matunda mpaka sasa ni;

Tulimwita Ofisa Biashara wa Mkoa Kagera, Naibu RAS Tendega na Ofisa Kilimo, nao walikuja na kufika mahali pa mauzo ila hawakutusaidia.

Tulifika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa Agosti 2023 kumweleza tatizo hili, naye alimwita mnunuzi na kumwamuru RPC amweke chini ya ulinzi, lakini licha ya kufuatilia, pakawa na ukimya, hatukujua hatima na mwafaka.

Vilevile, tulifunga safari hadi Ofisi ya Waziri Mkuu jijini Dodoma. Tulielekezwa na Dk. Stanley Gowele kuonana na Dk. Rupia ambaye tulikaa naye kikao ofisini kwake na kumweleza changamoto za malalamiko, alitusikiliza na kutuhakikishia kuwa Waziri Mkuu atalipatia ufumbuzi kwa rejeo la barua ya tarehe 09/10/2023 tuliyowasilisha kwake.

Hatukuishia hapo, tulifika pia ofisini kwa Waziri wa Kilimo baada ya kukosa mwelekeo Desemba 4, 2023, naye akatukabidhi kwa Mkurugenzi wa Wizara na tumefuatilia tunaahidiwa suala letu litafanyiwa kazi lakini hadi leo ukimya umetawala.

Tulimwandikia barua tena Waziri Mkuu Februari 2024 na kujibiwa barua tarehe 14 Febrauri 2024, wanasema suala hili limeelekezwa Wizara ya Kilimo, tunaambiwa tuendelee kuwa na subira.

Pamoja na ahadi hiyo, tunaona suala letu limekwama kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kutolishughulikia kwa kuwa Wizara ya Kilimo haijatuelekezwa ni nani mhusika wa kushughulikia jambo hili.

Tunapofuatilia Wizara ya Kilimo, inasema tayari taarifa yao kupitia tume maalum imewasilishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na huku Ofisi ya Waziri Mkuu ikisema suala hilo liko Wizara ya Kilimo.

Ndugu mhariri, wakulima tunaodai malipo hayo tuko 856.

Tunamwomba Mheshimiwa Rais kutusaidia wakulima wa vanila Mkoa wa Kagera kulipwa fedha zetu kwa sababu ni muda mrefu sasa kampuni haijatulipa.

Kama hatuwezi kulipwa, tunaomba Mheshimiwa Rais atusaidie turudishiwe vanila zetu tutafute soko wenyewe.

Pia tunamwomba Mheshimiwa Rais kutuma timu ya kuichunguza kampuni hii kuona kama ilikuwa na uwezo wa kununua vanila za wakulima kama ilivyoidhinishwa na uongozi wa Mkoa wa Kagera kwamba ina uwezo wa kununua vanila.

**Stevene Ntwara**
**Mwenyekiti Msaidizi**
**Umoja wa Wakulima wa Vanila Kagera**
**S.L.P 61, Kagera**
**0659 920311**


# Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationships beyond banking*

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions) (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

**A. REMITTANCE –OUTWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

**B. REMITTANCE –INWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

**C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES**

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | – | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | – | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | – | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | – |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

**D. Other Common Charges**

| Item | Charges | |
|---|---|---|
| | **TZS A/c** | **USD A/c** |
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

**E. CLEARING SERVICES**

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| | **TZS A/c** | **USD A/c** |
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection - USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

**CREDIT MATTERS**

| | Charge/Fees |
|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher.<br>**Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**2) Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** |

| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD Facility<br>USD 5 | TZS Facility<br>TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | |
|---|---|
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

**OTHER DISCLOSURES**
**(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 04.04.2024 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 04.04.2024 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 04.04.2024 |

# Mbunge: Kuuza malighafi ni kujitangazia umaskini milele

## ●Bajeti ya SU iwe sehemu ya bajeti kuu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Vwawa, Japhet Hasunga ameitaka serikali kuangalia uwezekano wa kujumuisha bajeti za mashirika ya umma katika bajeti kuu.

Amesema kujumuisha huko kutalisaidia Bunge kupata mamlaka kamili ya kuyasimamia, akisisitiza hatua hiyo italeta tija katika maendeleo ya taifa letu.

Vilevile, mbunge huyo ametoa tahadhari ya uuzaji wa malighafi kwamba ni kujitangazia umaskini wa milele.

Mbunge huyo aliyasema hayo bungeni Dodoma alipochangia mjadala wa mapatio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kupitia R4 za Rais Samia Suluhu Hassan, serikali inaweza kukaa chini na kuona namna ya kufanikisha suala hilo.

"Katika bajeti iliyopo kuna bajeti ya serikali kuu ambayo ni Sh. trilioni 33, serikali za mitaa Sh. trilioni 1.3 mashirika ya umma hakuna, misaada ya mikopo Sh. trilioni 5.1, mikopo ya nje Sh. trilioni 9.6, hiyo inajumuisha bajeti ya Sh. trilioni 49. Ukiangalia hapo bajeti za mashirika ya umma hazipo na ndio zinatekeleza majukumu ya serikali," alisema.

Hasunga ambaye kitaaluma ni mhasibu, alisema kuwa mwaka 1996, Robert Smith alikuja na mwongozo wa bajeti ya serikali kuu katika kuitayarisha, akisema inahitaji kuwa na vyanzo vya mapato.

"Akaweka masuala ya kodi, akaondoa bajeti ya mashirika ya umma na taasisi zake zote, akasema hizo zote zisisiingie kwenye bajeti kuu.

"Matokeo yake nchi nyingi zikaiga mfumo huo, sasa kila bajeti kuu inayokuja unakuta mashirika mengi ya serikali na taasisi zake hayapo katika bajeti kuu.

"Mapato yote ambayo yanakusanywa, iwe TTCL, bandari, TRC bajeti zao haziendi bungeni kwa sababu ya hiyo kanuni. Sasa imefika wakati serikali ikae iangalie ile kanuni kama bado ina umuhimu wa kuendelea kubaki kama ilivyo au kuna haja ya kuiangalia upya ili bajeti za mashirika ya umma ziweze kuwa sehemu ya bajeti kuu," alisema.

Akizungumzia viwanda, Hasunga alisema maendeleo ya nchi yanapimwa kwa vitu vingi, mojawapo ni eneo hilo, akisisitiza serikali inapaswa kuwa na mkakati wa kutosha kuwa na viwanda mama vya kuongeza thamani.

Alisema viwanda vya kuongeza thamani bado havijapewa kipaumbele cha kutosha, hali aliyotaja imekuwa inachangia matatizo makubwa katika nchi.

"Wataalamu wanasema kama umeamua kuwa mazalishaji malighafi, maana yake umechagua kuwa maskini wa milele. Hatuwezi kuendelea kuwa wazalishaji wa malighafi.

"Sasa hivi tunazalisha mazao mengi tunayoyauza kama malighafi ikiwamo pamba, kahawa, korosha, chai, haitupeleki mahali pazuri kama nchi lazima tuhakikishe tunakuwa na viwanda vya kuongeza thamani na kutengeneza bidhaa za mwisho.

"Hapo ndio tutaona thamani ya viwanda na tutakuwa na uchumi wenye manufaa na nchi, tutamaliza tatizo la ajira sasa hivi kila kitu tunaagiza nje, hii siyo.

"Kwahiyo, serikali ina haja kukaa chini na kuangalia katika viwanda mama tunafanyaje, na vile vya kuongeza thamani, hapo ndipo tutafanikiwa," alisema.

Kuhusu biashara, Hasungu ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), alisema biashara za ndani na nje hazifanywi vizuri kwa sababu serikali imejikita katika kuuza malighafi, kitu ambacho si kiashiria kizuri kwa maendeleo ya taifa.

Pia alitaka serikali kutenga fedha kwa ajili ya kurekebisha barabara zilizoko katika eneo lake la kazi, akibainisha kwamba ndio kikwazo kikubwa cha kusafirisha mazao ya chakula yanayolimwa huko.

"Kule kwetu sisi (Vwawa) ni wazalishaji, tunalima kahawa na mazao ya chakula kwa wingi, tuna tatizo la miundombinu ya kusafirisha, ni shida, tumekuwa tunapiga sana kelele lakini hakuna lililofanyika.

"Ninaiomba serikali iziangalie sana zile barabara ili bidhaa zinazozalishwa zisafirishwe na kuchangia Pato la Taifa," Hasunga alisema.

Kuhusu huduma za jamii, mbunge huyo alisema kunahitajika kufanywa msawazo katika ugawaji rasilimali kwenye maeneo ya viwanda, biashara na upande wa huduma za jamii ili kujenga rasilimaliwatu na uchumi mzuri.

"Mbali na maeneo hayo, kuna eneo la watumishi wa umma, hawa wanalipa kodi, wanatakiwa wapate mishahara mikubwa, wakilipwa vizuri ndio makusanyo ya kodi yanakuwa makubwa na wao wanakwenda kutumia fedha zao kuwekeza na kufanya biashara, kodi inaongezeka na mzunguko wa fedha unakua, angalieni maslahi ya watumishi wa umma na sekta binafsi ndipo uchumi wetu utakua," alisema.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Etaro, wilayani Musoma mkoani Mara, wakijifunza kwa vitendo katika maabara ya shule hiyo, mwishoni mwa wiki, baada ya kupata vifaa vya maabara hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miradi ikitekelezwa vizuri, lawama kwa CCM zitaisha

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani, AbdulSharifu Zahoro amesema miradi ya maendeleo ikitekelezwa kulingana na fedha zilizotolewa, itasaidia kuondoa lawama kwa wananchi na maswali katika uchaguzi ujao na chama hicho kuibuka na ushindi.

Amesema halmashauri zikizingatia kujenga miradi kwa ubora unaotakiwa kama ilivyo kwa Halmashauri ya Chalinze, wananchi watanufaika na utatuzi wa kero kwenye maeneo husika.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati Kamati ya Siasa ya chama hicho ilipofanya ziara ya siku moja kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo.

"Maeneo mengine wajifunze Halmashauri ya Chalinze inavyotumia mapato ya ndani kutekeleza miradi bora, ikumbukwe wananchi wakikosa huduma nzuri, lawama wanazielekeza CCM na endapo watatatuliwa kero zao na huduma bora zikapatikana, hakutakuwa na malalamiko," alisisitiza Zahoro.

Kamati hiyo ilipongeza watendaji wa halmashauri hiyo kwa usimamizi wa miradi ambayo imetekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na ujenzi wa soko la Bwilingu ambalo limegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.4 likiwa na vizimba 230 na fremu za maduka 37, kwa sasa lipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Katika mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi alisema umejengwa kwa fedha za ndani na lengo ni kuongeza vyanzo vya mapato na wafanyabiashara wadogo kupata sehemu salama ya kufanyika shughuli zao.

Pia katika duka la dawa lililojengwa Kituo cha Afya Chalinze, Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Allen Mlekwa alisema limejengwa kuongeza upatikanaji bidhaa za afya kwa wateja na kupunguza usumbufu kwenda kutafuta dawa katika maduka ya nje.

"Duka hili pia litapunguza gharama za matibabu kutokana na kwamba bei ya bidhaa za afya katika duka la jamii ni nafuu kulinganisha na bidhaa za afya katika soko," alisema.

Dk. Mlekwa alisema kuwapo duka hilo pia kutaongeza kipato kwa kituo hicho ambacho kitatumika kuboresha utoaji huduma za afya na kwamba hadi sasa ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 41.3, makadirio hadi kukamilika mradi huo yakiwa Sh. milioni 46.1.

Miradi mingine iliyokaguliwa ni ujenzi wa Shule ya Msingi Ridhiwani Kikwete na jengo la wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya Miono, miradi ambayo kamati hiyo pia iliridhishwa na utekelezaji wake.


UBALOZI WA MAREKANI, UINGEREZA, FINLAND NA INTERNATIONAL COMMITTEE OF RED CROSS DAR ES SALAAM

MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani, Uingereza, Finland, na International Committee of Red Cross watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Fanicha, GYM equipments na Generator **tarehe 13 April, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Chest drawer, Meza za garden, Viti, Book case, Dresser, Meza za ofisi, Viti, Steel cabinets, Fridge double door, Deep freezer, Washer, Dryer m/c, Majiko ya umeme na Gas, Laptop, Computer sets, A/c split unit, safe, Ngazi na pipa za taka (Trush cans) Simtank 5,6,8,15,Ltrs na vingine vingi.

**Magari, Genereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Toyota Land Cruiser Hard Top | 1HZ Diesel Engine | 2018 | Haujalipwa |
| 1 | Toyata Land Cruiser Hard Top | 1HZ Diesel Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Pick Up | 1HZ Diesel Engine | 2007 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Hard Body Double Cabin | CD22 Diesel Engine | 2010 | Umelipwa |
| 3 | Generator 5KVA & 500 KVA | Perkins Diesel Engine | 2001 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 8 mpaka 12 April 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 19 April, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**



## Mwenge wa Uhuru kuzindua miradi ya bil.40/-

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MWENGE wa Uhuru umeanza kukimbizwa mkoani Tanga, huku ukitarajia kuzindua miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 40.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian, alisema mwenge huo ukiwa katika Wilaya ya Korogwe utakagua na kuweka mawe ya msingi katika miradi 87.

Alisema mwenge huo unatarajiwa kukimbizwa umbali wa kilomita 1635 na baada ya kupitia miradi na kuikagua, utakabidhiwa mkoani Morogoro

Aidha, alisema kwamba fedha hizo zipo kwenye mchanganuo wa Sh. bilioni 40.9, nguvu za wananchi ni Sh. milioni 196.8, halmashauri Sh. bilioni 1.8, Serikali Kuu Sh. bilioni 20.8, fedha za wahisani Sh. bilioni 18.4 ambazo zimepelekea kuwepo kwa idadi hiyo wa fedha hizo.

"Ujumbe maalumu wa mwenge mwaka huu ni tunza mazingira na shiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ujenzi wa taifa endelevu. Kwa hiyo tunategemea kwenye miradi ya mwenge kutakuwa na utunzaji wa mazingira, kutakuwa na ujumbe wa kupiga vita dawa za kulevya" alisema.

Kadhalika alisema pamoja na ujumbe huo, Mwenge wa Uhuru utaendelea kuhamasisha na kuwaelimisha wananchi juu ya mapambano dhidi ya rushwa, malaria, Virusi Vya Ukimwi (VVU), UKIMWI, dawa za kulevya na uzingatiaji wa lishe bora.

Hata hivyo aliwataka wananchi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kuupokea mwenge wa uhuru pindi utakapopita katika barabara, kwenye miradi na maeneo ya mikesha.

**Alisema mwenge huo unatarajiwa kukimbizwa umbali wa kilomita 1635 na baada ya kupitia miradi na kuikagua, utakabidhiwa mkoani Morogoro**

# Wawili mbaroni tuhuma kutorosha mifugo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo, kimekamata watuhumiwa wawili wilayani Longido mkoani Arusha, wakitorosha mifugo 514 kwenda nchi jirani, huku wakitumia vibali vya kampuni isiyohusika na mifugo hiyo.

Kamanda wa kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Simon Pasua, akizungumza jana jijini Arusha, alisema mifugo hiyo ilikamatwa Aprili 6, mwaka huu katika Wilaya ya Longido.

"Aprili 6 mwaka huu, Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo chenye makao yake makuu hapa Arusha, kwa kushirikiana na baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Longido, tumefanikiwa kukamata mifugo 514, ikiwemo mbuzi na kondoo iliyokuwa inasafirishwa kwenda nje ya nchi, kwa kutumia kampuni ambayo haihusiani na mifugo,"alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Pasua, majina ya watuhumiwa hao kwa sasa yamehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi na kuomba wananchi kutoa taarifa za watu wanaojihusisha na utoroshaji wa mifugo na kukiuka taratibu za uuzaji wa mifugo nchini na inayokwenda nje ya nchi.

Kamanda Pasua alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kufuata taratibu za uuzaji wa mifugo, ili kutokukumbana na mkono wa sheria na kulikosesha Taifa mapato.

Alisema jeshi hilo limejipanga kikamilifu kudhibiti wizi wa mifugo na litaendelea kuwakamata wale wote watakaokiuka taratibu za uuzaji na usafirishaji wa mifugo, hasa inayokwenda nje ya nchi.

Alisema: "Kuanzia sasa wafanyabiashara wa mifugo, hakikisheni mnapotaka kusafirisha mifugo yenu kwenda nje ya nchi, mnatimiza taratibu zote ikiwemo vibali, ili kuepuka usumbufu ikiwa ni pamoja na kukamatwa".



Baadhi ya wakazi wa wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wakiwa wameshika miche ya miti wakijiandaa kupanda katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya kata ya Potwe, jana, wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Polisi: Usithubutu kufanya uhalifu Sikukuu ya Eid El-Fitr

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga limetangaza mapambano dhidi ya watu watakaothubutu kujihusisha na vitendo vya uhalifu katika Sikukuu ya Eid El-Fitr.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Tanga, Almachius Mchunguzi, alitoa angalizo hilo na kusema wamejipanga kuhakikisha hali ya usalama inakuwapo mkoani hapa.

Alisema kuwa Jeshi la Polisi limejipanga kikamilifu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa kufanya doria ili kukabiliana na wahalifu.

Alisema wamejipanga kwa kufanya doria za miguu, magari na pikipiki katika sehemu za ibada na kumbi za starehe, kuhakikisha wananchi wanasherehekea sikukuu kwa amani.

Kadhalika, aliwaomba wananchi kusherehekea Sikukuu ya Eid El-Fitr huku wakilinda mali zao nyumbani Ili kuepuka kuibiwa .

# Mvua yakatisha mawasiliano Barabara Arusha- Namanga

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAWASILIANO ya Barabara Kuu ya Arusha/ Namanga inayokwenda katika mpaka kati ya Tanzania na Kenya, yamekatika kwa zaidi ya saa nne, baada ya mvua inayonyesha kujaza kifusi cha tope chenye urefu wa mita 300.

Aidha, usiku wa kuamkia jana barabara ya kuelekea Olmot Sekondari daraja lake lililojengwa hivi karibuni limesombwa na maji na kusababisha wananchi kukosa mawasiliano.

Jana, Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Arusha, Reginald Massawe, alisema eneo lililoathiriwa zaidi ni njia panda ya Ngaramtoni, ambako mafuriko yameng'oa madaraja, kufanya uharibifu kwenye makazi ya watu pamoja na mashamba makubwa ya wawekezaji.

"Jana usiku (juzi) majira ya saa 5-9 imenyesha mvua kubwa sana katika eneo la Ngaramtoni na eneo la Odlonyosambu na imeleta maji mengi sana yameporomoka kutoka milimani, yamekuja kwenye barabara yetu kuu ya Arusha-Namanga.


"Hapa tuliposimama (anaonyesha) panaitwa Sakina, maji yamekuja mengi sana yamepita juu ya kalavati. Yote yaliyokuwa yamejengwa yakiwa na tope kubwa sana na baadhi ya magogo yamesombwa huko na kusababisha barabara hii kuwa na tope kubwa sana.

..Tumekagua kipande chote eneo la mita 300 limeathirika na tumeshaanza tuko na mkandarasi tunazoa tope na tutaendelea kufanya ukaguzi wa maeneo yote ambayo maji yametoka huko milimani ili tuweze kuona hatua stahiki za kuchukua

Haya maji yameenda hadi Arusha bypass na kufanya uharibifu wa kilomita nne, yanasomba udongo wa pembezoni mwa barabara na maji ni mengi sana na yanasababisha mmong'onyoko mkubwa na tunaendelea kujenga kuta za mawe katika meneo ambayo yameathirika na mtaro wa kilomita mbili katika barabara ya bypass ili tuwe na suluhisho la kudumu." alisema.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Jamal Twalib, alisema walishtuka muda wa saa 9:00 usiku na kukutana na maji ya mafuriko.

Vilevile, Joel Mollel, alisema: "Sisi wafanyabishara hapa tunapata hasara maduka yamejaa maji vitu vimeharibika tunapata shida serikali iangalie uboreshwe miundombinu na wala serikali haiwezi kutusaidia kama kwangu ofisi ya saluni ya kunyoa na kutengeneza sabufa za watu zimejaa maji."





# TTCL kuja kivingine utoaji huduma za intaneti

**Na Rose Jacob,** MWANZA

BODI ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) imesema shirika hilo lipo kwenye mpango wa kufanya maboresho makubwa katika mtandao wa 'intaneti' ili kuongeza ushindani katika soko la mawasiliano ya mtandao wenye kasi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi mkoani hapa na Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL, Zuhura Muro katika futari iliyoandaliwa na shirika hilo na kusema lengo ni kufikia mahitaji ya watumiaji wa mtandao huo nchini.

Vilevile alisema uboreshaji huo utaenda sambamba na kuwekwa kwa huduma ya mtandao yenye kifurushi maalumu cha WiFi kwa matumizi ya familia.

Akizungumza katika futari hiyo kwa niaba ya Shekhe wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, Katibu wa Baraza la Masheikh mkoani hapa, Othuman Asasi aliwataka Watanzania kulinda amani ya nchi kwa kutambua na kufuata wajibu walionao katika imani zao.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala aliyemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alisema dhamira ya serikali ni kuona huduma za mawasiliano zinaimarika nchini.

Masala aliitaka shirika hilo kuendelea kufanya kazi karibu na wananchi kwa kubaini mahitaji yako na kuwahudumia ipasavyo ili kuhakikisha jamii nzima inafikiwa na huduma za mawasiliano kama yalivyo maono ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Masala alisema: "Rais anahitaji jamii ifikiwe mawasiliano yasiyo na changamoto yoyote kama ilivyo kwenye miundombinu ya barabara, afya, elimu na maji".




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (wa pili kushoto), akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (wa tatu kushoto), wakifanya ziara ya kukagua eneo la kitalu na 66 B, ilipojengwa Shule ya Msingi Makongoro, jijini Mwanza jana, lenye mgogoro baina ya Kanisa la AICT na Halmashauri ya Jiji hilo. **PICHA: ROSE JACOB**

# Waagizaji dawa watakiwa kuwa wazalendo, kufuata sheria

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAAGIZAJI wa dawa wametakiwa kufanya kazi kwa ubora, kutanguliza uzalendo, kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ili dawa hizo ziweze kutumika katika matumizi yaliyokusudiwa.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Dk. Thomas Rutachunzibwa wakati wa warsha iliyowakutanisha wadau wa uagizaji wa dawa kutoka Kanda ya Ziwa iliyofanyika Jijini Mwanza.

Alisema baadhi ya waagizaji wa dawa siyo waaminifu wanatumia njia za panya na kutopitia TMDA kwa ukaguzi wa dawa hizo ili kubaini kama zinafaa kwa matumizi ya binadamu.

Aidha, aliwataka kutotanguliza fedha katika kutekeleza majukumu bali wajali afya za watu kwa kuagiza bidhaa zenye viwango vinavyokubalika.

Alisema serikaki imeimarisha udhibiti ubora wa dawa katika maeneo ya mipakani kwa kuhakikisha hakuna dawa zinazoingia kinyume na utaratibu, huku doria imara katika bandari zote na maneno ya viwanja vya ndege zimewekwa wakishirikiana na wahudumu wa afya katika maeneo hayo.

Mkurugenzi Udhibiti wa Dawa kutoka TMDA, Daktari Yonah Mwalwisi alisema wadau hao ni watu muhimu lakini ni vyema wakawauzia wananchi bidhaa tiba kwa kufuata masharti na sheria za kuuza na kuagiza bidhaa tiba, ili zitumike katika makusudi yaliyowekwa na mamlaka hiyo

Alisema: "Wapo baadhi ya watu wamekuwa wakitumia vibaya dawa za uzazi na zinginezo kwa matumizi yasiyo sahihi hasa wale wanaonunua kwa lengo la kutoa mimba na kuwataka wauzaji wa dawa kutoa maelekezo stahiki kabla ya kuuza kwa wananchi kwa sababu dawa lazima itumike kwa lengo la kutibu na siyo vinginevyo".

Katibu wa Chama cha Waagizaji wa Dawa (TAPI), Abbas Mohammed ambaye alikuwa mmoja wa wadau wa warsha hiyo alisema mabadiliko ya teknolojia yanakwamisha shughuli nzima ya uagizaji na usambaji wa dawa.

Alisema mchakato wa usajili wa dawa hauendani na kasi ya maendeleo na madaliko ya teknolojia ya sasa katika kuhudumia wananchi ipasavyo.

Hivyo aliiomba TMDA iweke mifumo mizuri na rafiki katika kuzuia mianya yote ya kuagiza na kuingiza dawa kwa njia isiyo halali kwani inakwamisha ufanisi wa kazi kwao.

# Lyabukande wakubaliana kuwatenga wanaotekeleza ukatili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Lyabukande wilayani Shinyanga, wamepitisha maazimio ya kuwachukulia hatua watu ambao wanaendekeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuwafikisha katika vyombo vya dola pamoja na kuwatenga.

Miongoni mwa kundi hilo ni wazazi ambao bado wanaozesha wanafunzi ndoa za utotoni.

Maadhimio hayo waliyapitishwa juzi kwenye kikao cha majadiliano juu ya kuzingatia mila na desturi chanya zenye usawa wa kijinsi, kwa kuzuia vitendo vya ukatili zikiwamo ndoa za utotoni.

Kikao hicho kiliandaliwa na Shirika la WEADO kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT-Trust).

Walisema kutokana na baadhi ya wazazi katika kata hiyo ya Lyabukande kuendekeza vitendo vya kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni licha ya kuchukuliwa hatua za kisheria, pia Jamii inapaswa kuwatenga kama adhabu na kukomesha kabisa vitendo hivyo

"Adhabu hiyo itakwenda pia kwa wanaume ambao wamekuwa wakiwapiga wake zao, kuwa licha ya kupigwa faini na Serikali ya Kijiji Sh.100,000 na mifuko miwili ya saruji wao pia wanapaswa kupewa adhabu ya kutengwa na Jamii." walieleza.

Diwani wa Lyabukande, Luhende Kawiza, alisema wananchi wanaogopa kutengwa na jamii kuliko kupigwa faini na ndiyo maana wamepitisha maadhimio hayo ambayo yatasaidia kumaliza vitendo vya ukatili zikiwamo ndoa za utotoni.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Lyabukande, Salumu Hamisi, alisema kutokana na jamii kuendekeza mila na desturi kandamizi hasa mfumo dume, wamekuwa wakipokea kesi nyingi za wanawake kunyanyaswa kiuchumi na waume zao, zikiwamo na ndoa za utotoni.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko, alisema wanatekeleza mradi wa 'chukua hatua sasa zuia ukatili' kwenye kata hiyo ya Lyabukande, wakianza na kutokomeza mila na desturi kandamizi, kwa jamii yenyewe kupitisha maadhimio hayo ambapo watawachukulia hatua wale ambao hufanya ukatili.

Aidha, Mratibu wa Mradi kutoka shirika hilo, John Eddy, alisema jamii inapaswa kubadilika na kuacha kuendekeza mila na desturi ambazo zimeshapitwa na wakati, ili kutosababisha vitendo vya ukatili wa kijinsi bali waishi salama na kuzingatia mahitaji ya usawa katika nyanja zote.



Ukurasa 12

ELIMU SOKONI

**Darasa teknolojia kuvusha wajasiriamali, kisha kupenya kimtandao hadi sokoni**



Ukurasa 13

MRADI DREAMS

Tiba darasa inayoelekezwa penye hatari HIV kwa vijana, kinamama


Nipashe

# TESA

Jumanne Aprili 9, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 14

**Wanyama tisa wanaoishi muda mrefu bila ya chakula wala maji**

ELIMU

NA PETER ORWA

# Mwalimu na mwanafunzi walivyo majibu ya kwanza kupaa elimu

JUMANNE wiki iliyopita katika safu ya makala hizi ilikuwa na tafsiri pana ya nguzo zinazoshika elimu ya mwanafunzi hata kufanikisha, ukiwapo ubia wa nguzo nne kitaifa: serikali, shule, wazazi, wadaiwa umma kwa jumla ukibeba tafsiri pana na inayohusu mambo mengi.

Lakini, inaporejewa kwa kina, kufanikiwa elimu kunazama katika nguzo kuu mbili; mwalimu anayewasilisha maarifa na ufundi, upande wa pili ni wake mwanafunzi mpokeaji.

Wakati mlengwa mkuu ni mwanafunzi mpokeaji wa ujuzi na maarifa hayo, pacha hao mwalimu na mwanafunzi wanakuwa kama wachezaji mpira uwanjani kufanikisha elimu inayofuatiliwa na kila kona duniani.



Mwalimu akiendelea na jukumu lake darasani. **PICHA: MTANDAO**

Staili ya Mwalimu anakuwa ana muhtasari wa masomo kwa siku hiyo, akilenga kuingiza kichwani mwa mwanafunzi. Ni kawaida kabla hata hajafanya kazi hiyo mwalimu sahihi anakuwa kajijenga na darasa lake, akiwafahamu wanafunzi kisaikolojia, tabia, utashi na mazingira yao kwa kikundi, pia mwanafunzi mmoja mmoja.

Vilevile mwanafunzi, ama kwa mazoea au kufunzwa anajiandaa taratibu, kanuni, mbinu za somo na mahitaji ya mwalimu, anapoingia darasani kwake.

Hapo inaambatana na kanuni na sheria, kama vile mavazi ya sare na adabu za darasani.

Ndipo mbia mwalimu anajiweka sawa na kuanza 'kushusha nondo' alizoandaa huku mara zote akiongozwa na tathmini akihoji kama wako pamoja na ndio chimbuko la maswali 'are we together?'.

Iwapo watu hao hawajaka sawa, aanendesha ushirikiano wa mdomoni na ubaoni, hata wakati mwingine masihara yenyue uhusiano na mada hiyo, hata uelewa kwa wanafunzi ukafikiwa. Ndio chanzo wakatui fulani mwalimu wa Chekechea au darasa la pil anaingia katika mchezo wa kitoto.

Kisaikolojia uso wa binadamu huongea, pia anayekwama anaonekana kwa ishara ya machoni, kusuasua kuandika, au anayelewa anakuwa na mtazamo au ishara kinyume na hayo, akitikisa kichwa, majibu ya 'ndiyooo!' na kadhalika.

Mwalimu ndani ya uwasilishaji wake unakuwa amegawanya mada ya siku hiyo ndani ya hatua akioanisha na mifano mikuu inayofanana na maisha ya wanafunzi, hata wanakuwa wepesi kudaka kinachofunzwa. Lingine ni ufunzaji wa mwalimu, unaendana na kipimo cha umri na ndipo hapo mahali muhimu zaidi, kwani staili ya kujifunza darasani la kwanza, iko tofauti sana na darasa la saba.

'Iwe isiwe' ni eneo muhimu zaidi linalomrudisha mwalimu chuoni, katika masomo kama falsafa, saikolojia na usimamizi wa darasa, huku binadmu wa taaluma hiyo, mbinu za tathmini zikichukua nafasi yake.

Mbali na tathmini ya jumla, mwalimu huwa na na tathmini ya majumuisho juu ya kile anachofundisha kama vile kutoa mazoezi ya kufanya. Kwa mwalimu wa masomo ya sayansi au ufundi, kuna wakati darasa linahaa maabara au 'workshop'.

Mwanafunzi mara zote anasimama katika kutimiza maelekezo ya kisheria na kitaaluma, ambayo yana kawaida kumfungulia milango ya uelewa kitaaluma.

Lakini, mafanikio hayo yana 'vigezo na masharti' muhimu katika kufanikisha elimu. Kwanza, ni nidhamu ya jumla na mahsusi ya utekeleaji majukumu hayo kielimu, kwa mwalimu na wanafunzi.

Pia, mwalimu na mwanafunzi kufanikiwa darasani ni sehemu moja, lakini kutimizwa kwa mahitaji kama vyumba vya madarasa, samani zake, idadi ya walimu, bajeti sahihi na mitaala sahihi, vyumba vya maabara ni mambo muhimu.


**INAENDELEA WIKI IJAYO**

TEKNOLOJIA
NA SHABAN NJIA,
KAHAMA

ELIMU NDANI YA SOKO

# Darasa teknolojia kuvusha wajasiriamali, kisha kupenya kimtandao hadi sokoni

UJASIRIAMALI katika sura ya uchumi, inamaanisha kuwezesha ajira kupatikana. Wajasiriamali wanatajwa kuwa muhimu katika kukuza pato la taifa. Mchango wao unatajwa kuongezeka maradufu.

Licha ya kuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa watajwa bado hawana elimu ya kutosha katika utengenezaji bidhaa zenye ubora, hata kumudu ushindani sokoni ndani na nje ya mipaka.

Hivyo, Chama cha Wafanyabiashara wanawake Tanzania (TWCC) kimeanzisha utaratibu wa kuwatembelea wajasiriamali nchi nzima kuwapatia elimu ya uzalishaji bidhaa ubora, zenye sifa ya kushindana ndani ya Soko Huru la Afrika (AfCFTA).

Ni elimu inayotolewa kwa kushirikiana na taasisi za serikali, ikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirikisho la Wafanyabishara Viwanda na Wakulima (TCCIA), GS1, PASS Leasing Company, kwa ufadhili wa Trademark Afrika (TMA).



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita (kushoto), akizungumza na wajasiriamali wakati wa ufunguzi wa mafunzo yao, kuhusu kanuni, taratibu na sheria za kufanya biashara kwenye soko huru la Afrika (AfCTA. **PICHA: SHABAN NJIA**

### MKURUGENZI WAO

Mwajuma Hamza, Mkurugenzi wa TWCC, anasema, wajasiriamali wanawake wamekuwa wakizalisha bidhaa kulinganisha na wanaume, lakini zinakosa ubora wenye masoko makubwa na ndio nafasi kwao kujipatia fedha.

Anasema, utafiti wamegundua kundi la wajasiriamali wanawake wanazalisha bidhaa zisizokuwa na ubora unaoweza kushindaniwa kwenye soko huru la Afrika na ndio sababu inayowafanya kutoa elimu, kuondokana kuwa tegemezi kwenye jamii.

Mwajuma anasema, mkoa wa Shinyanga wamefanikiwa kuwafikia wajasiriamali zaidi ya 100 wanachama na wasio wanachama wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake.

Hao wanaelimishwa, namna ya kutengeneza bidhaa bora na wanatoka Kishapu, wilaya ya Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama.

"Soko huru la Afrika lina zaidi ya ushindani wa wajasiriamali bilioni 1.2 kutoka nchi 54 na ili tuweze kushindana nao na kupata masoko. Huko lazima tuwe na bidhaa zilizokidhi vigezo kutoka katika mamlaka zetu nchini, najua tunazalisha bidhaa nyingi ila hatuna elimu inayotuongoza kwenye ushindani sokoni," anaongeza.

> "Nipende kuwashukuru TWCC kwa kuandaa mafunzo haya kwa wanawake. Fursa hii itawawezesha kujua masoko ya bidhaa mbalimbali ikiwemo ya Afrika Mashariki.

Anaongeza, kila mwaka wamekuwa wakiwafikia wajasiriamali hao milioni moja ili kuwapatia ujuzi nchi nzima na sasa wametoa elimu kwa wajasiriamali wanawake 100, ili kuwa na bidhaa zitakazoshindana katika masoko huru Afrika.

### FURSA WIZARANI

Mwajuma anasema, hivi karibuni alikaa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, akafahamishwa tayari wizara hiyo imeanzisha mfuko maalumu wa kudhamini wafanyabiashara; wakubwa, kati na wadogo wakipata fursa kwenye masoko ya nje, hivyo kila mmoja achangamkie fursa.

Anataja sifa ya kupata fursa, kila mjasiriamali katika kuandaa au kuunda wasifu wa biashara yake anayoifanya, ambazo wataziwasilisha wizarani, ili wapate msaada kupitia mfuko huo na watakaokidhi vigezo hasa, vya kuwa na bidhaa watakaonufaika na mfuko huo.

Anasema, tayari wana masoko nje na wamekosa mitaji ya kuzalisha bidhaa nyingi na kupeleka nje, pia wizara itawasaidia kupitia mfuko huo.

Wameanzisha soko la mtandaoni, litakalotumika kutangaza bidhaa zinazotengenezwa na wajasiriamali maeneo mbalimbali, ili waweze kupata masoko ya nje kirahisi.

### VIONGOZI NA WALENGWA

Katibu Tawala Msaidizi, Biashara, Viwanda na Uwekezaji mkoani Morogoro Beatrice Njawa, anasema ili kufikia malengo ya kufikisha bidhaa katika masoko ya nje, ni vema kukaundwa timu ndogo itakayosaidia kinamama.

Ni suala linalohakikisha wanafikia soko huru la Afirika, kuhudumia nchini 54 na itakuwa changamoto zao.

Anasema, kwa kutumia Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), wajasiriamali hao watakaoweza kuyafikia malengo yao, kwa sababu watakuwa wanakumbushwa kila mara.

Misingi ya kutengeneza bidhaa zenye ubora, anaamini wanawake waliopata mafunzo hayo watayotumia ipasavyo, kama fursa kwa kujua masoko ya bidhaa wanazozalisha.

"Nipende kuwashukuru TWCC kwa kuandaa mafunzo haya kwa wanawake. Fursa hii itawawezesha kujua masoko ya bidhaa mbalimbali ikiwemo ya Afrika Mashariki.

"Hasa kwa kuzingatia ukuaji wa viwanda unaotegemea upatikanaji wa malighafi na ukuaji wa masoko," anaongeza Njawa.

Mboni Mhita, Mkuu wa Wilaya ya Kahama anawataka wajasiriamali hao kuchangamkia fursa za mikopo isiyokuwa na riba ya asilimia 10, iliyokuwa ikitolewa na halmashauri awali, kwani sasa serikali imeweka utaratibu mzuri ili zitolewe na taasisi za kifedha zitakazoainishwa baadae.

Anasema, hatua ya mikopo hiyo kutolewa na taasisi za kifedha, imekuja baada ya kuwapo kwa malalamiko kwa baadhi ya wajasiriamali kutaka iwe inatolewa, pia kwa mjasiriamali mmoja mmoja, badala ya kwenye vikundi pekee na serikali imesikiliza ombi hilo hivyo ukosefu wa mtaji, ambao ni msingi wa kibiashara umetatuliwa

Sada Jumanne, miongoni mwa wajasirimali 100 wa mkoa Shinyanga, waliopewa elimu ya kutengeneza bidhaa zenye ubora unaohitajika kwenye soko huru la Afrika, anasema wanazalisha bidhaa nyingi sokoni ni la ndani na wateja watakaotafuta, kupitia kwa rafiki wenye simu janja.

Mjasiriamali kutoka kata ya Nyihogo, Manispaa ya Kahama, anasema kikundi chao wamekuwa wakizalisha unga lishe, kwa ajili ya kukabiliana na utapiamlo kwa Watoto, lakini wanakosa soko la uhakika.

Bidhaa wanalalamika kuna wakati inaharibika kwa kukaa ndani muda mrefu na kupata hasara ya gharama wanazotumia.

### WENYEVITI TWCC MIKOA

Makamu Mwenyekiti wa TWCC Taifa, Rose Romanus, anasema, kwa sasa kuna mazingira mazuri ya kufanya biashara, kwa wajasiriamali kulinganisha na ilivyokuwa hapo awali na kuwataka kutumia nafasi kuyafikia masoko yalipo na ili kuyafikia, kila mmoja anatakiwa kutengeneza bidhaa zinazokidhi viwango na sio vinginevyo.

Anasema, soko huru Afrika lina ushindani mkubwa na wajasiriamali kutoka mataifa 54, hivyo ni lazima kuwa na bidhaa bora, kwani bidhaa zisizosajiliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na taasisi nyingine haziwezi kupata soko.

Rose anasema, mkoa unaofanya vizuri katika mashindano ya Juakali, unapaswa kuendelea kuitendea haki, kwa kuwa na bidha zenye ubora unaohitajika kwa kuzingatia mafunzo yaliyotolewa, ikiwamo na kujielimisha kwenye biashara zao kwa kutafuta masoko.

Mwenyekiti wa Mkoa wa Shinyanga, Joyce Egina, anasema wamekuwa wakizalisha bidhaa nyingi kulingana na fursa zilizopo, ila baadhi zinapata masoko ya uhakika katika mazao la mpunga, mahindi, viazi lishe, korosho na kunde, zikipata soko katika jirani za Rwanda, Uganda, sudani kusini na Kongo.

ELIMU

NA GRACE MWAKALINGA, KYELA

UJUE MRADI WA DREAMS

# Tiba darasa inayoelekezwa penye hatari HIV kwa vijana, kinamama

• Aliyefikwa, asimulia alivyosota kufika ng'ambo



Sehemu ya utekelezaji mradi wa Dreams, mkoani Mbeya. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA tatizo la mmomonyoko wa maadili, kuna sababu inayotajwa vijana kujiingiza katika vitendo vya kihalifu na kujiweka katika mazingira hatarishi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, kunatajwa chanzo mojawapo ni hali yao duni ya kiuchumi.

Ukosefu wa vyanzo stahimilivu vya kuwaingizia kipato, inatajwa ni kikwazo katika maisha yao, ikisababishwa na kufiwa na wazazi au walezi, wakiachwa bila uangalizi kuwapelekea kuwa na maisha duni na uhitaji wa huduma za msingi kwenye maisha yao.

Miongoni mwa vijana hao ni, Tina (sio jina lake), mkazi wa kijiji cha Masebe, kata ya Mwaya wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, amepitia hayo kimaisha hali, hata anakiri akadumbukia kwenye ukahaba.

Binti huyo ameokolewa kutoka kwenye changamoto hizo na Mradi wa Dream, unaotekelezwa na Shirika la HJFMI, baada ya kutumbukia kwenye shida ukahaba.

"Mimi ni mtoto wa tano katika familia ya watoto sita, kwa bahati mbaya kutokana na maambukizi ya virusi vya ukimwi nilipoteza dada zangu watatu na kubakia binti pekee na kaka zangu wawili," anaeleza.

Anafafanua, kutokana na vikwazo katika maisha, baba yake akawaambia wabaki na mama yao, ambaye hakujimudu kwani hakujimudu kujishughulisha, kutokana na maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.

Pia, anasema kaka yake akaanza kuugua maradhi ya akili, mwingine akijiingiza kwenye makundi hatarishi akitumia pombe, dawa za kulevya na wakathirika kisaikolojia.

Kutokana na matatizo yaliyoikumba familia yao, ilimbidi afanye kila kitu kuhakikisha wanakula na kupata mahitaji yote muhimu ya nyumbani na ya kwake binafsi.

Anasema haikuwa rahisi kupata pesa, hivyo alilazimika kufanya ngono ili apate pesa ya kulisha familia na yeye kukidhi mahitaji yake kama mtoto wa kike.

Katika hali hiyo, anasimulia akapata ujauzito ambao baba wa mtoto aliukataa kutoka na tabia aliyokuwa nayo ya kuwa na wanaume wengi, hata akalea peke yake na kujifungua mtoto njiti.

"Baada ya kujifungua mtoto njiti, hali yangu ya kimaisha ikawa ngumu zaidi, kwa sababu ilihitajika pesa nyingi kumlea mtoto huyo, huku familia ikinitegemea mimi kwa kila kitu.

"Sikuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote cha kuniingizia pesa hapo ndipo mkombozi wangu Dreams alipokuja," anaeleza mama huyo.

### HATUA MABADILIKO

Anafafanua katika mizunguko yake, akakutana na muelimisha rika aliyemueleza kuhusu mradi wa Dreams, huduma wanazotoa na kazi wanazozifanya, hata akawaunganisha na kikundi kiitwacho Masebe Super Women, alikopata elimu sahihi, iliyomsaidia kubadili fikra na kuamua mambo.

Anasema elimu ya mabadiliko ya tabia ilikuwa nguzo iliyombreha sana, hata akarejea nafsui ya tengeneza alivyo sasa kuwa binti anayejitambua.

Hapo wakampeleka katika kituo cha afya alikopata uduma za uzazi wa mpango na matibabu mengine, baadaye akapelekwa katika Chuo cha Ufundi - Veta kupata ujuzi na kozi ya lugha Kiingereza, inayomuwezesha kuwasilina kwa stadi hiyo kwa ufasaha.

Mama huyo anasema, hadi sasa ameshanufaika akiwa na fursa mbalimbali kupitia mradi wa Dreams, akishiriki warsha na mafunzo ya kujengewa uwezo ndani na nje ya nchi, ikamfanya kuwa binti imara anayejitambua na kuwasaidia wengine kuepukana na tabia hatarishi.

Huyo ni miongoni mwa mabinti na wanawake vijana 130,000 walionufaika na mradi wa Dreams tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya.

### BOSI MUWEZESHAJI

Mkurugenzi wa Shirika la HJFMRI, Sally Chalamila anasema, mradi wa Dreams ulianzishwa kutekeleza afua mbalimbali za kupambana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kwa kuwasaidia walio katika rika balehe, wanawake na vijana walioko hatarini kupata maambukizi.

Anasema, Idara ya Ulinzi ya Marekani anayoitaja kwa jina WRAIR/DOD iliamua kufadhili miradi inayosaidia mapambano dhidi ya VVU ikiwemo na Dreams.

> Ukitaka kupata taswira ya maambukizi ya VVU, angalia wanawake, kwa sababu ndio wanaopata maambukizi kwa kiasi kikubwa, ukilinganisha na wanaume.

Anaufafanua ni mradi unaolenga kutoa kunusuru umma dhidi ya maambukizi ya VVU na waliopata watengeneze huima hiyo, kutengeneza mtandao utakaowasaidia wasiwaambukize wengine.

"Ukitaka kupata taswira ya maambukizi ya VVU, angalia wanawake, kwa sababu ndio wanaopata maambukizi kwa kiasi kikubwa, ukilinganisha na wanaume,"anatanka Chalamila na kuongeza kuwa, jamii inapaswa kuangalia namna inaweza kuwafikiwa wanawake wote, vijana na mabinti.

### WASAMBAZA MITAJI

Licha ya Shirika la HJFMRI kuweka nguvu katika kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi, vilevile limekuwa likiwajengea uwezo mabinti, wanawake na vijana kuelimika na ujasiriamali, wakiwapeleka vyuo vya ufundi kupata ujuzi aina mbalimbali na kuwakabidhi vifaa kwa ajili ya kuongeza thamani ya malighafi zao, wakijiingizia kipato.

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Wanyama tisa wanaoishi muda mrefu bila ya chakula wala maji


Simba wa Bahari


Buibui


Kobe


Nyangumi


Mamba

CHAKULA ndio chanzo kikuu cha nishati kwa mwili wa viumbe hai kufanya kazi vizuri, ikiwezesha usagaji chakula na kuipa nguvu mifupa, misuli na mishipa ya fahamu. Lakini kuna wanyama mashujaa, wanaoweza kuishi muda mrefu bila kula chakula au kunywa maji.

Wanyama wengine wanahitaji kupata milo kadhaa, ili kupata nguvu ya kuishi. Ngamia, wanaweza kuishi kwa miezi kadhaa bila maji na kuna wanyama wengine wanaofanana naye.

Pata orodha ya mashujaa tisa wanaomudu mfumo wa maisha kuzidi ngamia:

**1. Mamba:** Ni mmoja wa viumbe wakongwe duniani, anayeweza kuishi kwa miezi kadhaa bila ya chakula na wakati mwingine katika hali mbaya, anaishi hadi miaka mitatu bila chakula.

Wanahifadhi nishati kwa kupunguza harakati na wakati mwingine huacha kuzurura.

**2. Chura:** Wao hupatikana zaidi kwenye maeneo yenye unyevu, na miili yao inaweza kukaa bila ya chakula hadi miezi 16 au kwa lugha nyingine zaidi ya mwaka mmoja na robo.

**3. Buibui:** Wao kimaisha wanasubiri chakula chao kufika, miili yao imeundwa kwa namna kukaa miezi mitatu hadi minne bila ya chakula, uvumilivu kufika mwaka mzima.

**4. Kobe:** Kibaiolojia anaishi muda mrefu zaidi na anapofika ukubwa zaidi hutinga hadi uzito wa hadi kilo 417 akiwa na usugu wa kuishi bila chakula na maji kwa hadi mwaka.

**5. Simba wa Baharini;** Hao ni aina wanaoweza kuishi bila chakula kwa muda wa wiki nane hadi 10.

**6. Nyoka:** Nao wanaweza kuishi bila chakula kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hiyo inawezeshwa na ukweli kwamba, mfumo wao wa utumbo hupungua kwa asilimia 70 katika hali ya hewa ya baridi.

**7. Nge;** Nge hula theluthi moja ya uzito wa mwili wao kwa mlo mmoja. Hiyo inawasaidia kupunguza kemia ya mmeng'enyo wa chakula na kudhibiti lishe yao, hata kuifanya iwe rahisi kwao kukaa bila chakula kwa mwaka.

**8 Nyangumi:** Wenyewe hutumia mafuta ya ziada wanayohifadhi kila wanapokula wakati wa msimu wa joto, jambo ambalo huwawezesha kukaa bila chakula kwa hadi miezi sita nusu mwaka.

**9. Paka:** Ujasiri wake katika mlo, anaweza kuishi wiki mbili tu bila ya chakula. Ingawa paka huonekana anapenda chakula, wanaweza kuamua kutokula na kukaa bila chakula kwa hadi wiki mbili kulingana na afya zao au ikiwa mlo wao wa mwisho ulikuwa wa kuridhisha.

***Kwa mujibu wa BBC***

# Tiba darasa inayoelekezwa penye hatari HIV kwa vijana, kinamama

**INATOKA UK.13**

Mwezi uliopita, shirika HJFMRI kupitia mradi wa Dream, unaoendeshwa na asasi ya Tumaini, walitoa msaada wa vifaa vya kisasa kwa mabinti balehe na wasichana vijana wa wilaya ya Kyela, kuwawezesha kuzalisha bidhaa za nguo, viatu na sabuni na bidhaa nyingine.

Kupitia utaratibu wa kuwawezesha mabinti, HJFMRI imetoa vifaa ambavyo ni vyerehani vya kisasa vya kushonea nguo mashine 80, mashine maalum ya kudarizi nguo za kisasa 16, kunakishia nguo nane, kufuma kwa mkono sita, kukamua mafuta ya alizeti moja, kutengeneza sabuni moja, kutengeneza viatu viwandani mbili mashine ya kunakishia viatu nane vifaa hivyo vina thamani ya shioingi milioni 178.

Akizungumzia kuhusu mradi wa Dreams, mtaalamu wa masuala ya kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi VVU, kutoka Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi (PEPFAR) kupitia taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Jeshi la Marekani WRAIR/DOD, Dk. Alick Kayange, kuna mafanikio katika kukabiliana na Ukimwi.

Anasema utafiti uliofanywa mwaka 2016/2017 na kurudiwa mwaka 2022/2023 unaonesha mafanikio kutoka asilimia 55.7 hadi 87.4 walijua hali zao za maambukizi na kuanzishiwa dawa za kufubaza VVU na wale ambao wameanza matibabu imeongezeka kutoka 53.1 hadi 84.6 kwa mikoa ya Nyanda za juu kusini ikiwamo Mbeya.

Mratibu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania TACAIDS, mkoa wa Mbeya, Emmanuel Petro anasema kwa kushirikiana na Shirika la HJFMRI, mezinufaisha kata 89 zilizopo jijini Mbeya, Mbarali na Kyela wakitoa huduma kwa wasichana balehe na wanawake na waliojifungua katika umri mdogo.

Anafafanua kuwa mabinti wanapata afua za kitabibu, kimuundo na kitabia kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa kushirikiana na vituo vya afya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela,Florah Luhala anasema mabinti 20,000 wamenufaika na fursa mbalimbali zikiwemo za matibabu, ujuzi na elimu inayowawezesha kukabiliana na maambukizi mapya ya VVU.

Anasema katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wadau hao, halmashauri ilitoa mikopo wa sh. milioni nane kwa vikundi viwili kufanya shughuli za ujasirimali aidha wamepewa eneo ekari 17 kwa ajili kilimo cha kokoa na kuanzisha kiwanda cha kuchakata zao hilo.



# Mipango ya matumizi ardhi 63 yaandaliwa Chamwino

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) imepanga kutoa elimu ya masuala ya ardhi katika Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, ambapo mipango ya matumizi ya ardhi 63 imeandaliwa.

Msimamizi mradi huo Wilaya ya Chamwino mkoani hapa, Grace Mbena, aliyasema hayo jana wakati wa uhamasishaji wanachi kushiriki umilikishwaji ardhi.

"Tukio hili la kuhamasiha wananchi kushiriki katika zoezi la umilikishaji ardhi limejumuisha vijiji vitatu kutoka katika Wilaya ya Chamwino ambavyo ni Iringa Mvumi zamani, Iringa Mvumi na Cheta ambapo wananchi walifanya shughuli mbalimbali ikiwemo kucheza ngoma "alisema Mbena.

Aidha, alisema wataendelea na uhamasishaji huo katika vijiji vilivyobakia kwa kuwa lengo ni kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi 80, kuboresha uhusiano kati ya timu ya utekelezaji mradi pamoja na wananchi wa wilaya hiyo, ili kutekeleza kazi hizo kwa pamoja.

Naye, msimamizi wa masuala ya kijamii na kimazingira wa mradi, Alpha Mangula, alisisitiza kuwa lengo kuu la kuandaa tukio hilo ni kutoa elimu juu ya umilikishwaji na utoaji wa hati miliki za kimila, haki za umiliki wa ardhi kwa wanawake na makundi mengine maalumu kama wazee, walemavu, vijana na watoto.

lengo lingine ni kuwezesha wananchi kutambua umuhimu wa kushiriki vikao vya uhamasishaji na kuwepo maeneo yao wakati wa utambuzi wa vipande vya ardhi.

Mmoja wa wananchi kutoka Kijiji cha Iringa Mvumi, Said Sulemani, alisema kuwa tukio hilo limewaleta wananchi pamoja na kuwahidi kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa ardhi.

Mradi huo unatekelezwa chini ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ukiwa na lengo kuu la kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa kuzingatia masuala ya kijamii na kimazingira.

Kwa maeneo ya vijijini mradi utatoa takribani hatimiliki za kimila 500,000 pamoja na vijiji 1,667 kuandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi.

# Mkuu wa Gereza akerwa wafungwa anaosamehe Rais kurudi gerezani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Gereza Kuu la Isanga mkoani Dodoma, ACP Zefania Neligwa, amesema anakerwa na tabia ya baadhi ya wafungwa ambao wamekuwa wakipata msamaha wa Rais, lakini baada ya kipindi kifupi wanarejea magerezani kwa uhalifu.

Aliyasema hayo jana baada ya kupokea msaada wa vyakula na vitu mbalimbali kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodona kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanawake wa Kiislam Tanzania (JUWAKITA).

Msaada huo ulitolewa kwa ajili ya wafungwa na mahabusu wa gereza la wanaume na wanawake Isanga kwa malengo ya kufuturu katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa na utaratibu wa kuwaachia wafungwa kwenye kila sherehe za kitaifa, lakini baadhi yao wamekuwa wakirejea tena tabia ambayo imekuwa ikikera na kuhuzunisha kwa kuwa msamaha huo walitakiwa kujirekebisha kitabia.

Alisema magereza yamekuwa sehemu kubwa ya kuwafanya watu wanaochukuliwa hatua za kisheria na kufungwa kuwa eneo la kujirekebisha tabia ili wanapoachiwa na msamaha au kumaliza kifungo wawe raia wema kwa jamii.

"Inapofikia hatua ya kuachiwa kwa msamahaa au kumaliza kifungo chake mimi pamoja na uongozi mzima wa magereza tumekuwa tukiwapa nasaha za kuwafanya wanaporudi huko majumbani waweze kuwa raia waliojifunza kitabia na wanatakiwa kutumia fursa walizojifuza kwa maendeleao.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajabu aliwataka wafungwa na mahabusu walioko magerezani kutumia vyema mwezi wa Ramadhani kwa ajili ya kutubu na kuomba toba ya kweli ili Mungu awasamehe katika adhabu zinazowakabili.

Shekhe Rajab alisema kuwa katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani ni muhimu wafungwa na mahabusu waliofunga wakafuturu na kupata chakula kama ambavyo waliopo uraiani.

Naye Mwenyekiti wa BAKWATA, Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary alisema mahitaji hayo yaliyokabidhiwa wanaamini yataenda kuwasaidia wale ambao wamefunga kwa mwezi huu Ramadhani na hata ambao hawajafunga.

Hata hivyo, alitaja misaada hiyo iliyokabidhiwa kwa wafungwa na mahabusu kwenye gereza hilo kuwa ni pamoja na sukari, ndizi, viazi mviringo na vitamu, mavazi maharagwe na vitabu vya kujisomea.




Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu (mwenye koti jeusi), akikabidhi msaada wa vyakula mbalimbali kwa Mkuu wa Gereza kuu la Isanga, ACP Zefania Neligwa vilivyotolewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Wilaya ya Dodoma jana, kwa ajili ya mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa wafungwa na mahabusu. P**ICHA: PETER MKWAVILA**

# BAKWATA yakoshwa hatua serikali kudhibiti mfumuko

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Singida limeipongeza serikali kwa kudhibiti mfumuko wa bei katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani.

Limesema hali hiyo imewezesha wananchi kununua bidhaa mbalimbali vikiwamo vyakula kwa bei ya kawaida.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro alitoa pongezi hizo jana wakati wa futari, dua na pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan iliyoandaliwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, BAKWATA, wabunge, wanasiasa na wananchi.

"Tunaipongeza serikali kwa kuweza kudhibiti mfumuko wa bei kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani kwani tumefunga kwa furaha na amani bila tabu ya manyanyaso ya bei zisizo na utu kutoka kwa wafanyabishara wenye nia ovu na tamaa za kupitiliza," alisema.

Shekhe Nassoro akizungumzia siasa aliviomba vyama vya siasa kutumia vyema fursa waliyopewa ya kufanya mikutano ya hadhara kwa maslahi ya taifa na kwamba haipendezi kutumia lugha za matusi, kashifa.

"Mkuu wa Mkoa usisite kuchukua hatua dhidi ya watu watakaoitumia fursa hii vibaya na wala usiwaonee haya hata kidogo, sisi viongozi wa dini tuko pamoja," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alieleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba pato la mkoa limekua na la mwananchi mmoja mmoja.

Alisema wastani wa pato la mkoa limeongezeka kutoka Sh.trilioni 2.709 mwaka 2020/2021 hadi kufikia Sh.trilioni 3.196 na pato la mwananchi mmoja mmoja limefikia Sh. milioni 1.5 mwaka 2022/23.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho Mkoa wa Singida umepokea Sh. trilion 1.7 kutoka serikalini kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hata hivyo alisema katika kuwainua wananchi kiuchumi Sh. bilioni 3.06 zimetolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye uelemavu na Sh. bilioni 2.2 zimetengwa kwa ajili ya kuvikopesha vikundi hivyo pindi serikali itakapotoa mwongozo mpya.





# Wakulima Ludewa walia ukosefu soko la uhakika

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANACHAMA na viongozi wa vyama vya ushirika wilayani Ludewa mkoani Njombe, wameiomba serikali kuwapa kipaumbele katika ununuzi wa mazao yao, ili kuwa na soko la uhakika.

Walitoa ombi hilo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva katika kikao kazi na vyama vya ushirika wilayani hapa.

Mmoja wa wanachama wa AMCOS kutoka Kijiji cha Shaurimoyo, Yohana Mhagama alisema wanaiomba serikali kupitia kitengo cha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) pindi unapofika muda wa ununuzi wa mahindi vyama hivyo vipewe kipaumbele.

"Tunaomba unapofika wakati wa uuzaji mazao ya mahindi kwenye utaratibu wa kununua mazao kupitia hifadhi ya chakula basi wavione vyama vya ushirika kuwa ndiyo jicho la kwanza, ili kuleta chachu kwa wakulima kuona umuhimu wa kujiunga na vyama hivyo," alisema Mhagama.

Naye Mwenyekiti wa AMCOS Kata ya Luilo, John Ngatunga alisema ucheleweshaji wa viuatilifu kumesababisha kushuka kiwango cha uzalishaji wa korosho.

"Nalia na nyinyi viongozi wa wilaya naomba kujua tatizo ni nini? kuna changamoto nyingi lazima nizitaje hapa kwanza kuna ucheleweshwaji mkubwa wa viuatilifu na upatikanaji wa dawa aina ya sulphur," alisema Ngatunga.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva alisema lengo la kikao kazi hicho ni kutathmini mwelekeo wa vyama vya ushirika wilayani humo vilipotoka, vilipo na vinapoelekea ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na kilimo chenye tija.

"Yote tuliyojadili leo ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na kilimo chenye tija, Rais Samia Suluhu Hassan ametupendelea Ludewa maofisa ugani wetu wote wana pikipiki za kuweza kufika mashambani ili kuweza kutupa huduma za ugani, lakini tumepata vipima udongo tunavitumia na tutaendelea kuvitumia," alisema Mwanzivva.

Alisema changamoto hizo zitafanyiwa kazi ili kuhakikisha wakulima wanakuwa na kilimo chenye tija na kupata matokeo chanya yatakayochangia kuinuka kwa uchumi.

"Hatutaki kurudi nyuma, tunataka kusonga mbele tunataka kilimo chenye tija, chenye faida tunataka kuona wakulima wetu wakifaidika, wakinufaika," alisema Mwanziva.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius alisema watahakikisha wanatatua changamoto za wakulima pamoja na kukuza uzalishaji wa kahawa.

"Kahawa ni moja ya mazao ya kimkakati katika halmashauri yetu na tayari tumeanza kuchukua ujuzi kwa jirani zetu Mkoa wa Mbeya ambao tuna uhakika utatuletea mabadiliko chanya katika kilimo chetu," alisema Deogratius.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Ludewa, Godfrey Mlelwa alisema kuhusu soko la mahindi wanunuzi wakubwa ni NFRA, lakini kwa upande wa vyama vya ushirika kumekuwa na changamoto kidogo.

Alisema NFRA wanaangalia njia nzuri ya kuwawezesha vyama vya ushirika kupeleka mazao yao.

Mrajisi wa vyama vya ushirika mkoani Njombe, Edmund Masawe aliwataka wanachama wa vyama hivyo kujisajili katika mfumo ili waweze kupata fursa mbalimbali ikiwemo masoko na mikopo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Rogath Robert akizungumza katika mkutano unaohusu madhara ya afya ya akili, mjini Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC: Vijana njooni mlime viazi mviringo muuage umaskini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa amewataka vijana kujitokeza wilayani kwake ili kuwekeza katika kilimo cha mazao ya muda mfupi, ikiwemo viazi mviringo ili kujikwamua kiuchumi.

Kasongwa aliyasema hayo wakati akizindua kongamano lenye lengo la kueleza fursa kwa vijana wilayani hapa ambalo liliwakutanisha wadau wa taasisi mbalimbali ikiwemo za kilimo na mifugo.

Kasongwa alisema Wilaya ya Njombe inafursa nyingi ambazo asilimia kubwa ni kilimo.

"Fursa zilizopo Njombe kwa asilimia kubwa ni kilimo, najua kwamba vijana tunapenda pesa za muda mfupi kwa hiyo tuwewaletea fursa za mazao ya muda mfupi kuna viazi, maharage, nyanya, ngano. Kwa hiyo vijana tuhakikishe tunaingia kwenye fursa hizi," alisema Kasongwa.

Aidha, aliwataka vijana kuhakikisha wanajikita katika kilimo ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

"Tutagawa mbegu za ngano tani 28 ikiwa ni moja ya mikakati ya kumuinua kijana," alisema Kasongwa.

Mkurugenzi wa EPD TECH, Lusajo Mwaihabi alisema vijana wengi wanafikiria kwenda mikoa iliyoendelea kiuchumi kama Dar es salaam kwa imani ya kuwa ndiko fursa zinakopatikana kitu ambacho siyo kweli.

Ofisa Biashara na Masoko kutoka kampuni ya Itracom Fertilizers Limited, Gabriel Kimaro alisema fursa namba moja ni ajira kwa sababu kampuni hiyo imeajiri vijana katika nyanja mbalimbali.

"Fursa ya pili ni kwa wale wanaomiliki maduka yao binafsi yanayojihusisha na uuzaji wa pembejeo za kilimo hawa nao ni kundi la wanufaika katika fursa ya uwepo wa kampuni yetu na fursa ya tatu ni wakulima ambao wananufaika kupitia mbolea zetu kwa kuvuna mavuno mazuri," alisema Kimaro.

Ofisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Fredy Kawogo aliwataka vijana kujikita katika kilimo cha zao la parachichi kwa sababu limekuwa likiwapa utajiri watu wengi.

Baadhi ya vijana akiwemo Barick Yohana aliliambia Nipashe kuwa kongamano hilo limewaongezea ujuzi ambao hapo awali walikuwa hawavijui hususani kwenye kilimo na ufugaji.

# Wanaopika aina moja ya chakula wamkera RC Mtaka

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka ametoa wito kwa wananchi wa Kata ya Utalingolo Halmashauri ya Mji Njombe kuachana na utamaduni wa kupika chakula cha aina moja kila wakati, ili kukabiliana na tatizo la udumavu.

Mtaka aliyasema hayo wakati akizungumza kwa njia ya simu na wananchi wa Kata ya Utalingolo katika uzinduzi wa kampeni ya kupamba na udumavu sambamba na zoezi la ugawaji wa mnyama aina ya simbilisi.

"Bado tunafamilia ambazo wanapika makande wanakula wiki nzima, wanapika viazi wanakula wiki nzima, lakini vyakula hivyo vinatumika katika familia ambazo zinalima aina tofauti ya vyakula," alisema Mtaka.

Hivyo, alitoa rai kwa wananchi wa Utalingolo kuzingatia mlo kamili kwenye familia.

"Mlo kamili hautoki mbinguni, mlo kamili ni mahindi tuliyonayo unayasaga hakuna haja ya kula sembe, usage mahindi uweze kula dona kwa sababu panya anakula kiini cha hindi na binadamu anakula kapi la hindi," alisema Mtaka.

Mtaka alibainisha kwamba watoto wa Utalingolo wengi wao wanalo tatizo la upungufu wa uzito kwa maana ya ukondefu.

"Lakini wengine wanapata shida kubwa ya udumavu wa akili, mtoto anafundishwa darasani haelewi wakati mwingine ndiyo hao wakati wa ukubwa kwenye majukumu wanashindwa hata kuendesha familia kwa hiyo haya yote yanahitaji mlo kamili," alisema Mtaka.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Erasto Mpete, alisema wananchi wanapaswa kula nyama ya simbilisi kwa wingi ili kupambana tatizo la utapiamlo, ukondefu na udumavu.



## USAID: Uwepo viwanda vya mwani utaongeza thamani ya zao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Misaada la Marekani (USAID) limesema uwepo wa viwanda vya kuchakata mwani kutaongeza thamani ya zao hilo na wakulima ambao asilimia 90 ni wanawake.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Craig Hart alipowatembelea wakulima wa mwani eneo la Bweleo Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Hart alisema wamefanya utafiti na kubaini wakulima wa mwani wanahitaji kuwepo kwa viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya zao hilo kwa ajili ya mahitaji mengine ya ziada.

Alipongeza juhudi za wakulima ambao wamehamasika katika kulima kilimo hicho vijijini katika maeneo yaliyopakana na bahari.

Alisema kazi kubwa inayofanywa na USAID ni kuwawezesha wakulima hao kupata mbinu za kisasa za kilimo hicho pamoja na utaalamu na kuwapatia fedha za kuendeleza shughuli za uzalishaji.

"Tunaviomba vikundi vilivyoomba fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mwani kuhakikisha wanazingatia mafunzo ambayo yatawawezesha kupata mbinu mpya za kisasa za kuendeleza kilimo hicho"alisema.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wakulima Zanzibar, Hamad Hamad alisema tayari vikundi sita wameviwezesha na kuwapatia fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mwani kuingia katika mbinu mpya za uzalishaji wake.

Alisema ili wakulima wafikie viwango vya kuzalisha mwani, wanahitaji kupata mbinu mpya za kisasa ambazo zitawawezesha kulima kwa tija kufuatia kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya kilimo hicho, ambapo sasa hulimwa katika kina kikubwa cha maji.

Mkurugenzi wa Idara ya Mazao na Uvuvi wa Bahari, Dk.Makame Ali Shauri alisema hakuna sababu kwa nini kilimo cha Mwani kisilete mageuzi makubwa na kuwa mkombozi kwa wakulima kwa sababu tayari serikali imeonesha njia za kuyafikia malengo.

Alisema tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kuongeza thamani ya mwani eneo la Chamanangwe Pemba ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani za mwani 30,000 kwa mwaka.

# Bei ya vitunguu maji Z'bar yafikia 13,000/- kwa kilo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya vyakula na viungo visiwani Zanzibar zimepanda maradufu katika kipindi cha kuelekea Sikukuu ya Eid El- Fitri, ambayo inatarajiwa kuanza ndani ya wiki.

Bidhaa hizo ni vitunguu maji, kwamba kilo moja inauzwa Sh. 13,000 kutoka Sh. 4,500.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi walisema ni kawaida kwa wafanyabiashara inapokaribia kipindi cha sikukuu kupandisha bei kwa visingizio tofauti.

Fatma Bakari kutoka Mjini Unguja alisema anashangaa kuona bei ya kitunguu maji imepanda, hasa ikizingatiwa kuwa bidhaa hiyo na zingine huwa na mahitaji makubwa katika kipindi cha sikukuu.

Aliitaka serikali kusimamia bei elekezi kwa bidhaa zote ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi hasa wanyonge ambao baadhi yao hushindwa kumudu gharama kubwa za maisha.

Nipashe ilitembelea baadhi ya masoko ikiwemo la Mwanakwerekwe, Darajani, Jumbi na Makufuli kushuhudia upandaji wa bei za bidhaa, huku baadhi ya masoko hayo yakiwa hayaingiliki kutokana na kuzingirwa na maji kulikosababishwa na mvua inayonyesha.

Katika masoko hayo, Nipashe lilishuhudia kitunguu swaumu kilo moja inauzwa kwa Sh. 12,000 ambapo wiki moja iliyopita bei ya bidhaa hiyo kwa kiwango hicho iliuzwa kwa Sh. 6000.

Baadhi ya wafanyabiashara katika masoko hayo walisema bei za bidhaa zimepanda hasa vitunguu maji kwa sababu ya kuadimika.

Walisema Zanzibar inategemea bidhaa hiyo kutoka mikoa ya Tanzania Bara na baadhi ya mikoa inakabiliwa na changamoto ya mvua kubwa.

"Licha ya kupanda kwa bei ya vitunguu maji lakini pia vimeadimika sokoni hii inatokana na mvua kubwa zinazoendelea katika baadhi ya mikoa Tanzania Bara tunakotegemea kwa bidhaa hii" alisema Juma khamis mfanyabiashara wa Soko la Mwanakwerekwe.

Ofisa Msaidizi wa Soko la Mwanakwerekwe Unguja, Abasi Sururu Juma, alisema baadhi ya bidhaa zimeanza kuingia nchini kutoka Tanzania Bara ikiwemo vitunguu maji, lakini bei yake haitarajiwi kushuka kwa hivi karibuni kutokana na tatizo la usafirishaji.

"Bidhaa ya vitunguu maji vipo tumeanza kuvipokea kwa wingi kutoka Tanzania Bara lakini kumejitokeza tatizo la usafiri kutokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha katika baadhi ya mikoa yenye kuongoza kwa uzalishaji wake na kupelekea mfumo wa usafiri kuvurugika" alisema.

Alisema baadhi ya vitunguu vinaingia nchini kutoka India ingawa havikidhi mahitaji yake zaidi katika kipindi hiki cha kuelekea Sikukuu ya Eid-El-Fitri.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa soko hilo, Said Hamadi Ali alisema changamoto kubwa bado kuna mnyororo wa kodi ambazo hurudisha nyuma juhudi za wafanyabiashara wanapotoa bidhaa bandarini.

Hivyo, aliiomba serikali kupunguza mzigo wa kodi ili kuwarahisishia wananchi kumudu kununua bidhaa za vyakula katika kipindi cha kuelekea katika Sikukuu ya Eid-El-Fitri.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Bara, ambaye pia ni Waziri Mkuu Kivuli, Isihaka Machinjita, akishuka kutoka kwenye boti, alipokuwa katika ziara yake ya kutembelea waathirika wa mafuriko wilayani Rufiji, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Asasi za kiraia zatakiwa kuhamasisha uoteshaji mikoko

**Na Mwandishi Wetu**

ASASI za kiraia zimetakiwa kuongeza kasi ya kuwashawishi wadau kuotesha miti aina ya mikoko katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki Kisiwani Pemba na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Community Forest ya Pemba (CFP), Mbarouk Mussa wakati akizungumza wakati wa upandaji miti aina ya mikoko katika eneo la Kambini Wete.

Alisema taasisi hiyo tangu mwaka 2011 imekuwa ikijishughulisha na kuotesha mikoko katika maeneo ya pembezoni mwa bahari ambayo yapo katika tishio la kuvamiwa na maji ya bahari.

Aidha, alisema mbali na kazi za kuhamasisha upandaji wa miti ya mikoko taasisi hiyo imekuwa ikiwashawishi wananchi katika kilimo cha mboga pamoja na viungo kwa kugawa mbegu.

Alisema eneo la Kijiji cha Kambini ni miongoni mwa maeneo ambayo yameathirika na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa maji ya bahari kupanda juu, kufuatia changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Ofisa wa Idara ya Uvuvi Pemba, Suleiman Ali Hamad, alisema mikoko ni eneo mojawapo muhimu linalosaidia kuongezeka kwa mazalia ya samaki pamoja na viumbe vya baharini.

Alisema ukataji wa mikoko kwa kiasi kikubwa kumeathiri uzalishaji wa samaki katika Kisiwa cha Pemba ikiwemo samaki aina ya kamba.

Aidha, aliwataka wananchi wa Kijiji cha Kambani kuhakikisha wanalinda miti aina ya mikoko pamoja na maeneo yao yanakuwa salama na tishio la kasi ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman alisema serikali imeanza kutekeleza mikakati ya Zanzibar ya kijani kwa ajili ya kurudisha mazingira na kuotesha miti aina ya matunda.

Alisema katika kulinda mazingira wamejipanga kuotesha mikoko kwa wingi ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ambapo zaidi ya maeneo 150 yameathirika na changamoto za mazingira.

# EPZA, FSD Afrika zaingia makubaliano uwezeshaji kifedha maendeleo viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi ya (EPZA), imeingia makubaliano na taasisi ya Afrika ya FSD (Financial Sector Deepening) ili kufungua fursa na kuunga mkono uwezeshaji wa kifedha endelevu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya miundombinu ikiwamo ya maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) kuendana na Maendeleo Endelevu ikitumia teknolojia ya kijani.

Mkurugenzi wa Utafiti, Sera na Mipango wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Alfred Mkombo alisema makubaliano hayo kati ya EPZA na FSD Afrika ni hatua muhimu katika kujenga mfumo katika uwezeshaji kifedha wa miradi ya umma na maendeleo ya masoko ya mitaji.

"Mkataba huu unaongeza kujiamini hasa kwa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika masoko ya mitaji ili kupata fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miundombinu mbalimbali ya viwanda," alisema.

Alisema tangu kuanzishwa kwake, Mamlaka ya EPZ imekuwa ikiwezesha na kuhusisha kwa karibu sekta binafsi katika maendeleo ya viwanda kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje ya nchi.

Ili kutekeleza vyema mpango huu unaweka msingi wa mambo mawili, maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi (EPZ) ambayo mamlaka imekuwa ikizikuza na kutilia mkazo kwa ushirikiano na sekta binafsi na maeneo haya ni msingi wa maendeleo ya viwanda hasa katika kuongeza thamani kwenye bidhaa za viwandani.

"Makubaliano kati ya EPZA na FSD Afrika inatoa uhakika kuwa mpango huu wa uwezeshaji kifedha wa taasisi za sekta binafsi utakuwa na mafanikio makubwa," alisema.

Mkuu wa Ujumbe na Mkurugenzi wa taasisi ya FSD Afrika, Dk Evans Osano, alisema makubaliano kati ya EPZA na FSD Afrika ni mpango muhimu unaonesha jinsi Tanzania ilivyojizatiti kuchangamkia fursa za kupata fedha kupitia masoko ya mitaji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya viwanda kupitia maeneo ya SEZ.

Alisema mpango huu unaendana na mwelekeo wa kiulimwengu na masoko ya mitaji yanaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuwezesha kupata fedha na mitaji kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya kijani ya viwanda.

Alisema Uwekezaji wa Kijani unaunga mkono lengo la Mamlaka ya EPZA la kupata fedha kama njia mbadala ya kuwezesha kupata fedha na mitaji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya viwanda.

Osano aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kujenga uchumi imara kwa kuwa na mifumo thabiti ya kisheria ambayo huwavutia wawekezaji na kuwapa fursa na urahisi wa kuwekeza nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe alisema kupitia Wizara ya Fedha, serikali ilitoa miongozo ya namna ya kupata uwezeshaji kifedha mbadala na taasisi za umma zinaweza kupata mitaji kutoka kwenye masoko ya mitaji ili kuendeleza na kujenga miundombinu ya viwanda.

Njia hizi mbadala za kuwezesha kupata fedha na mitaji ni pamoja na hati fungani, mikopo maalum, ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi na pia kutumia fursa mbalimbali kutoka kwenye masoko ya mitaji.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Emmanuel Nyalali, aliahidi kuwa soko la hisa linaunga mkono na litakuwa kiunganishi muhimu kuisaidia EPZA kupata uwezeshaji kifedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya viwanda nchini.

Mkurugenzi wa Fedha wa Orbit Securities, Gideon Ligate alisema kuwa kuanzia sasa mfumo wa zamani wa namna ya kupata fedha za uwekezaji utaunganishwa na masoko ya mitaji ili kupata matokeo chanya katika uwezeshaji wa kifedha kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

## Mbolea feki yawaondoa kazini maofisa wanane

**NAIROBI,** Kenya

MAOFISA wanane wakuu katika Shirika la Kukadiria Ubora wa Bidhaa nchini Kenya (KeBS) wamesimamishwa kazi kutokana na kudaiwa kutoa vibali vya ubora kwa kampuni zinazosambaza mbolea inayodaiwa kuwa feki.

Ilielezwa kuwa watuhumiwa hao watakuwa nje ya maeneo yao ya kazi wakati wakisubiri uchunguzi unaoendelea kuhusu suala hilo unaofanywa na Ofisi ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Bunge.

Maofisa wa upelelezi nchini humo walisema wanane hao ambao walihojiwa na DCI kwa siku tatu mfululizo kuazia Aprili5, mwaka huu walizuiliwa kutokana na utoaji wa vyeti na nembo za ubora wa bidhaa kwa kampuni mbili, ambazo zimehusishwa na mbolea ya kiwango cha chini.

Hata hovyo, ilielezwa kuwa wapelelezi hao wamewataka maofisa kadhaa wa mashirika ya serikali ambao walishughulikia mbolea hiyo bandia ambayo inaendelea kuuzwa kufika katika ofisi zao.

Vile vile, walisema wamewaita wale wote wanaohusika na upatikanaji na usambazaji wa mbolea hiyo feki. Na kwamba timu hiyo imepanga kulifikisha suala hilo katika ngazi yoyote kabla ya kupeleka faili lao kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na mapendekezo mbalimbali. **BBC**



Maofisa wa uokoaji nchini Russia wakiwavusha wananchi kwenye maji baada ya kutokea kwa mafuriko katika miji miwili ya milima ya Ural, na kusababisha takribani nyumba 6,000 kuzingirwa na maji na kuwalazimu maelfu ya watu kukimbia makazi yao, juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Kanisa kusherehekea miaka 125

**Na Mwandishi Wetu**

WAAMINI wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo Matombo, mkoani Morogoro wanatarajiwa kusherehekea miaka 125 tangu kuanzishwa kwake ifikapo Oktoba mwaka huu.

Baada ya kuwaapisha wajumbe wa Kamati ya Jubilei ya miaka 125 ya kanisa hilo, Paroko wa Kanisa la Mtakatifu Paulo Matombo, Octaviani Msimbe alisema kanisa litasherehekea Jubilei ya miaka 125 mwaka huu.

Kanisa Katoliki la Mtatifu Paulo Matombo Morogoro linatarajiwa kufanyiwa ukarabati wa miundombinu iliyochakaa, ujenzi wa nyumba za parokia na ununuzi wa gari kwa ajili ya parokia hiyo.

Paroko Msimbe aliomba waumini, waliobatizwa wazaliwa wa Mkoa wa Morogoro na Watanzania kuchangia ukarabati wa kanisa hilo ambalo baadhi ya miundombinu imechakaa.

Alisema zaidi ya Sh. milioni 200 zinahitajika kwa ajili ya kufanya ukarabati wa kanisa hilo, ujenzi wa nyumba za mapadre na nyumba za masista.

Alisema majengo ya kanisa yamekuwa yanafanyiwa ukarabati mdogo kwa baadhi ya maeneo, lakini maeneo mengine yameonekana kuchoka, akitolea mfano paa la kanisa na baadhi ya majengo kuvuja.

Akizungumzia njia za utafutaji fedha, Mwenyekiti wa Kamati ya Jubilei, Robert Ruanda alisema wameanza kuchangisha waamini na kutengeneza kadi za michango za kuomba Watanzania kuwaunga mkono.

"Hadi sasa kiasi kilichopatikana kwa ajili ya shughuli hiyo ni Sh. milioni 16 katika ahadi ya Sh. milioni 29 kati ya Sh. milioni 200 zinazohitajika," alisema.

Kanisa hilo linahudumia zaidi ya waumini 700 na lilijengwa na Wajerumani.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akijadiliana jambo na Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge walia na sheria kikokotoo

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SAKATA la kikokotoo cha mafao ya wastaafu limeibuka tena bungeni, baadhi ya wabunge wakinyooshea kidole serikali kwamba ni kiini cha tatizo hilo.

Wamesema kikokotoo kipya kimeibua madhara makubwa kwa wastaafu, wakitaka kamati iundwe ili kupata ufumbuzi wa haraka.

Katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/25, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo alisema ni nia ya serikali kutaka suala la kikokotoo kufanyiwa kazi, hivyo ni jukumu la Bunge kuanza mchakato wake mapema iwezekanavyo.

Alisema Mei 202, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa ahadi ya kushirikiana na mihimili mitatu kulifanyia kazi suala hilo, hivyo Rais yuko tayari kuona mabadiliko ya kikokotoo kwa maslahi ya wastaafu.

"Nimepitia kanuni mbalimbali kama vile hii ya mwezi Mei 2022 ya Agosti 12, 2018, kanuni ya SCRA 2017 na 2018 pia na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge 2017 pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani ya 2017.

"Kikokotoo kilichokuwapo hadi mwaka 2014 kilikuwa ni kikokotoo kizuri na ndicho Watanzania wengi wanakitaka, chenyewe kilikuwa kimechukua asilimia 50 ambacho kilionesha miaka ya kuishi baada ya kustaafu kuwa ni 15 na nusu, pia kilichukua mshahara wa mwisho wa mfanyakazi ambao mara nyingi huwa ni mkubwa," alisema Gambo.

Vilevile, alisema kwa kikokotoo kimepunguza kutoka 1/540 hadi 1/580 pia wamechukua wastani wa miaka 10, wakitafuta miaka mitatu iliyo bora ambapo kwa kawaida lazima mshahara utapungua na kuathiri mafao, pia miaka ya kuishi imepunguzwa hadi 12, kitu alichodai si sahihi.

"Nimechukua mfano, sampuli ya mishahara na nimefanya mahesabu kwa mtumishi ambaye anastaafu akiwa na mshahara Sh. 800,000. Kwa kikokotoo cha kabla ya Julai 2014 katika mfuko wa LAPF na PSPF alikuwa anapata Sh. 57,466,666 na kwa kikokotoo cha sasa anapata Sh. 28,675,862 tofauti ya Sh. milioni 29,190,804. Kwa mwezi atapata Sh. 401,000 kwa kikokotoo cha zamani na cha sasa atapata 388,137," alisema Gambo.

Alisema katika hali ya kawaida kwenye kikokotoo hicho yamefanyika makosa makubwa kwa kuwa sheria inayoanzishwa inatakiwa kuanzia pale tu ilipotungwa. Kwahiyo, wote ambao sheria hiyo ilikuwakuta walitakiwa kulipwa kwa kikokotoo cha zamani na kipya kusubiri wale watakaoanza kazi.

Pia alitaka serikali kurejesha fedha zote ilizochukua katika mifuko ili kuirudishia uhai kama ilivyoshauriwa katika ripoti ya CAG, pia itenge bajeti kwa ajili ya kuinua mifuko hiyo na zitengenezwe kanuni mpya zisizowaadhibu wastaafu.

Mbunge wa Mbulu Mjini, Issay Paulo alisisitiza kurudi katika meza ya mazungumzo na vyama vya wafanyakazi kukipitia upya kikokotoo hicho kwa kuwa katika maeneo yake amekuwa akikutana na wastaafu wengi wanaolia juu ya suala hilo.

### KIFO CHA MBUNGE

Katika hatua nyingine Bunge hilo limeahirishwa hadi Aprili 15 mwaka huu kutokana na kifo cha Mbunge wa Kwahani, Ahmed Yahya Abdulwakil (CCM), aliyefariki dunia ghafla jana kwa shinikizo la damu, pia kupisha sikukuu za Idd El Fitir.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alitoa taarifa hiyo kwa Bunge jana jioni, akisema mbunge huyo alifariki jana na maziko yatafanyika leo kijijini kwao Buyuni, Zanzibar.

"Waheshimiwa wabunge kwa mujibu wa kanuni yetu ya 173 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kesho (leo) hakutakuwa na kikao cha Bunge ili kutoa fursa kwa wabunge kushiriki maziko, Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi... Amina," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 09/04/2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 09-04-2024 kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **DODOMA**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 18.00**
**Upana - mita 2.80**
**Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **DODOMA** kupitia **MOROGORO ROAD.**
Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# ACT yataka Majaliwa akaone uhalisia Rufiji

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimemtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani chini), afike Rufiji na Kibiti, mkoani Pwani kuona hali halisi na kuhakikisha hatua stahiki na haraka zinachukuliwa kunusuru wananchi waliokumbwa na mafuriko.

Kimesema mafuriko hayo yametokana na kuzidiwa kwa Bwawa la Mradi wa Kufua Umeme kwa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), hivyo kulazimika kuifungua milango minne ili kuyapunguza, jambo lililosababisha maji kufurika katika makazi na baadhi ya mashamba ya watu.

Mkoani Dar es Salaam jana, Waziri Mkuu Kivuli wa ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita alitoa kauli hiyo akitaka serikali kuweka mpango wa kukabiliana na maafa.

Mchinjita alisema matukio ya maafa na majanga kwa miaka ya hivi karibu yamedhihirisha uwezo mdogo wa serikali kuyakabili kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere tangu miaka ya nyuma ulitolewa tahadhari na mojawapo ilikuwa ni kudhibiti maji yasisababishe mafuriko makubwa na kuathiri wakazi jirani.

"Sasa Bwawa la Rufiji limejaa, ukisoma andiko la mradi linaeleza kutakuwa na mabwawa mengine ya kuhifadhia maji yakijaa.

"Serikali kwa kujiambia yenyewe bila kufuata taarifa za Mamlaka ya Hali Hewa (TMA) na wataalamu ikadhani itajaza bwawa hilo kwa miaka mitatu.

"Kwahiyo, wakaanza kujaza bila kuwa na hayo mabwawa ya akiba, matokeo yake mwaka huu kumekuwa na mvua kubwa, maji yamejaa kwa kiwango ambacho wakiacha bila kuyatoa litapasuka na litafunika Rufiji yote," alisema Mchinjita.

Alisema walichokifanya ni kuanza kuyafungulia maji na kwa sasa wamefungua milango minne inayomwaga maji mengi ambayo mpaka sasa yamejaza Bonde la Rufiji linalotumika kwa kilimo na sasa yanaelekea kuvamia makazi.

"Mashamba ya wakulima yote yamegeuka ziwa, sasa serikali imeanza kujitetea kwamba haihusiki, ninataka kusisitiza serikali inapaswa kuwajibika katika hili.

"Ukanda wa Kibiti na Rufiji eneo linalozunguka Bonde la Mto Rufiji, hasa lililoko karibu na bwawa la kuzalisha umeme kuna hali mbaya sana, zaidi ya kata 12 zimeathirika vibaya na maji, mazao, makazi, huduma za msingi za kijamii zimeharibiwa, wananchi wengi wamejihifadhi kwenye shule ambazo hazijapatwa na maji, hali ni mbaya," alisema.

Waziri Mkuu Kivuli alisema ni wazi ofisi ya maafa iliyoko chini ya Waziri Mkuu imeshindwa kuandaa utaratibu wa kukabiliana na dharura, pia matukio ya ajali zinazohitaji uokozi, akitolea mfano kuungua kwa masoko, ajali za moto, ajali za uokozi kwenye vyombo vya usafiri (ndege, treni).

Vilevile, alikumbusha serikali kuwalipa fidia waathirika 361 wa mabomu ya Mbagala, tukio lililotokea mwaka 2009 yaani miaka 15 iliyopita.

"Ni jambo la kusikitisha, kuona licha ya kucheleweshewa haki zao, wamekuwa wakipokea majibu ya kukatisha tamaa, kejeli na vitisho toka kwa watumishi wa serikali, wakiwamo wanaotoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Tunamtaka Waziri Mkuu kuhakikisha mwaka huu wanafuatilia suala hili na kuwafuta machozi waathirika hao kwa kuwalipa fidia ya haki.

"Hebu fikiria mtu anapewa fidia mpaka Sh. 1,400. Sasa hii atafanyia nini? Ni fidia ndogo sana, haiwezi kufanya kitu chochote," alisema.

Chama hicho pia kilitaka serikali kuweka mkakati madhubuti wa kukabiliana na majanga ikiwamo kununua vifaa vya kisasa vya uokozi.



Waziri Mkuu Kivuli pia alitaka serikali kuajiri walimu wa kutosha, akisisitiza kuwa upungufu uliopo ni wa walimu 279,202, idadi aliyoitaja si rafiki kwa ustawi wa sekta hiyo.

## ZISIKUPITE

### MARTIAL ATAKIWA INTER

INTER Milan wanaweza kumnunua fowadi wa Ufaransa, Anthony Martial, wakati mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, na Manchester United utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto - lakini ni ikiwa watashindwa kumsajili mshambuliaji wa Iceland, Albert Gudmundsson (26), kutoka Genoa. ***(Gazzetta dello Sport)***

### FATI AWINDWA WOLVES

KLABU ya Brighton haina nia ya kumnunua tena Ansu Fati baada ya uhamisho wake wa mkopo kutoka Barcelona, lakini Wolves, Valencia na Sevilla zinawezakuwasilisha ofa kwa mshambuliaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 21 msimu huu wa majira ya joto. ***(Sport)***

### CALVERT-LEWIN KUUZWA

KLABU ya Everton itahitaji zaidi ya pauni milioni 40 ili kumuuza mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### SZMODICS ATAKIWA LUTON

KLABU ya Luton imeonesha nia yao ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Blackburn na Jamhuri ya Ireland, Sammie Szmodics, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Brentford. ***(Sun)***

### ONANA KUONDOKA EVERTON

AMADOU Onana huenda akaondoka Everton msimu huu wa majira ya joto, huku 'The Toffees', wakitumai kupokea pauni milioni 50 hadi 60 kwa kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 22. ***(Football Insider)***

### AWANIWA BUNDESLIGA

KLABU za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, zina nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, kutoka Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott, 22, ambaye amekuwa akicheza kwa mkopo katika Klabu ya Excelsior ya Uholanzi msimu huu. ***(Football Insider)***

### BRANTHWAITE HANA MPANGO

MLINZI wa England, Jarrad Branthwaite, 21, amesisitiza kuwa anazingatia zaidi kushinda mechi na Everton na kwamba anapuuza uvumi wote kuhusu mustakabali wake wa muda mrefu, baada ya kuhusishwa na Manchester United, ***(Liverpool Echo)***

### MOTTA KUWA KOCHA JUVE

KLABU ya Juventus imefikia makubaliano kimsingi na Thiago Motta ambaye ni bosi wa Bologna kuwa kocha wao mpya - na kiungo wa kati wa Bologna na Scotland, Lewis Ferguson, 24, anaweza kumfuata hapo Turin. ***(Calciomercato)***

### ZANIOLO KUREJEA SERIAS A

WINGA wa Italia, Nicolo Zaniolo, anataka kurejea Serie A wakati mkopo wake kutoka Galatasaray kwenda Aston Villa utakapomalizika msimu huu, huku Fiorentina na Napoli wakiwa tayari wameulizia kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Gazzetta dello Sport)***

## DONDOO ... OKA MAGAZET ... AYA



# KLOPP: MBIO ZA UBINGWA KWA LIVERPOOL NI NGUMU

**MANCHESTER,** England

●●● Zitakuwa ngumu sana hadi mwisho, tulikuwa juu sasa ni Arsenal, tunataka...

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kiwango kilichooneshwa na timu yake hakitoshi katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Manchester United juzi, Jumapili.

**Kikosi cha Klopp kiliingia wikendi kikiwa na alama mbili zaidi katika mbio za ubingwa, na kilionekana kuwa tayari kudumisha faida hiyo kilipotawala kipindi cha kwanza dhidi ya United, ingawa kilipoteza nafasi nyingi.**

Lakini United walipambana na mabao ya Bruno Fernandes na Kobbie Mainoo yalimaanisha kuwa Liverpool walilazimika kutegemea penalti ya Mohamed Salah ili kuokoa pointi iliyohitajika sana Old Trafford.

Matokeo hayo yanaiacha Arsenal kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi huku Liverpool wakiwa nafasi ya pili kwa tofauti ya mabao.

Alipoulizwa kama anatarajia mabadiliko katika mbio za ubingwa, Klopp alisema: "Inawezekana ... lazima ushinde michezo mingi. Huwezi kufanya tulichofanya leo (juzi).

Hiyo haitatosha, hapana, lakini. Tunajua hilo. Bado, ikiwa unafanya kazi lazima uchukue tu vitu unavyopata.

"Niliona vijana wakitaka. Niliona timu kwenye mchezo mgumu wa ugenini. Timu nyingi huwa zinakuja United na watu wanajali zaidi, lakini kwetu kuja hapa ni mchezo wa kwanza, ni ngumu."

Liverpool wamekuwa katika mbio za ubingwa mara nyingi wakiwa chini ya Klopp, haswa mwaka 2022 wakati City na Liverpool zilikaa kwa miezi kadhaa bila kushindwa kabla ya timu ya Guardiola kushinda taji kwa pointi moja pekee.

Alipoulizwa ni kwa kiasi gani mwonekano wa jedwali la Ligi Kuu ni muhimu, Klopp alisema: "Ni muhimu baada ya mechi 38.

"Watu watatuambia tunatakiwa kusaka tofauti ya mabao, lakini hilo halifanyiki kwa makusudi, hauendi kwenye mchezo na kutaka kufunga mabao nane. Sisi ni hivi tulivyo, ndivyo tulivyo, na ndivyo hivyo, kwa nini tuko kwenye kinyang'anyiro, kwa hivyo nilijua kabisa kwamba itakuwa ngumu sana hadi mwisho.

"Tulikuwa juu; sasa ni Arsenal... tunataka kuwa hapo baada ya siku ya mwisho ya mechi."

# ARTETA: NIMESAHAU KUHUSU MWAKA JANA




**LONDON,** England

MIKEL Arteta amedai kuwa 'amesahau' kuhusu mwisho wa kusikitisha wa Arsenal kwa kampeni ya Ligi Kuu ya 2022/23 ambapo walimaliza kwa pointi tano nyuma ya mabingwa, Manchester City.

Arsenal walibwaga mbio za ubingwa wa taji la Ligi Kuu msimu uliopita mbele ya Man City walioshinda mataji matatu, licha ya kwamba 'Washikabunduki' hao kuna wakati walikuwa kileleni mwa jedwali kwa tofauti ya pointi nane.

Kocha wa Arsenal, Arteta anaamini kuwa msimu uliopita ni habari ya zamani, na anadai kuwa ameifuta akilini mwake.

Arteta aliulizwa kuhusu tofauti kati ya mwaka huu na uliopita na alisema: "Nadhani tuko katika wakati mzuri sana. Tuna kikosi kikiwa na afya njema na nguvu nzuri na kujiamini sana binafsi na kwa pamoja. Tunapaswa kuendelea tu kufanya kile tunachofanya.

"Kai Havertz hakika ana mchango mkubwa kwenye timu. Uchezaji wake kwa ujumla umekuwa mzuri sana na sasa idadi yake ya uchangiaji wa mabao iko juu sana. Anahitaji kudumisha hilo.

"Nadhani uelewa wake na wachezaji wa kushambulia ulikuwa mzuri sana. Nadhani walikuwa na lengo la kweli na muunganisho na uwazi mwingi wa wapi pakushambulia na tulitengeneza nafasi nyingi."

Alipoulizwa kuhusu msimu uliopita, maneno ya Arteta yalikuwa: "Nimesahau tayari."

Arsenal wanatumaini kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 20. Pia wapo kwenye Ligi ya Mabingwa na watamenyana na Bayern Munich katika mkondo wa kwanza wa robo fainali leo Jumanne.

# Cancelo ataka kubaki Barca



**LONDON,** England

JOAO Cancelo amedhamiria kupata uhamisho wa kudumu Barcelona wakati wa majira ya joto licha ya Chelsea, Arsenal na Bayern Munich kumuwindwa.

Beki huyo wa pembeni alijiunga na Barca kwa mkopo siku ya mwisho ya uhamisho wa majira ya joto, na amekuwa mchezaji muhimu kwa klabu hiyo tangu wakati huo. Cancelo ameichezea 'La Blaugrana' mara 32, na hivyo kuimarisha nafasi yake kama chaguo la kwanza la beki wa kushoto chini ya Xavi Hernandez.

Kwa mujibu wa Sport, Cancelo anataka kubaki klabuni hapo mara baada ya mkopo wake wa sasa kuisha, huku wakala wake Jorge Mendes kwa sasa akijaribu kusaidia kuwezesha mazungumzo kati ya klabu yake mama ya Man City na wababe hao wa La Liga ili kufanikisha hilo.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa City wamekuwa wakitaka kupata pauni milioni 40 kwa ajili ya huduma ya mchezaji huyo, huku Arsenal, Chelsea na Bayern Munich wakiwa miongoni mwa klabu nyingine zinazomuwania.

Inasemekana Barca walimwambia Cancelo kuhusu nia yao ya kutaka kumbakisha, jambo ambalo beki huyo wa pembeni alitarajia kulikubali.

Licha ya ofa anazoweza kupokea kutoka kwingineko msimu huu wa majira ya joto, Cancelo anabakia kuridhika na Barcelona na yuko imara katika nia yake ya kuendelea kucheza LaLiga.

Chaguo zinazozingatiwa kuongeza muda wa kukaa kwa Cancelo huko Katalunya ni pamoja na uhamisho wakati wa dirisha lijalo la majira ya joto, au mpango wa mkopo wenye chaguo la ununuzi linalofuata.

Juhudi zinaendelea ili kuangazia vikwazo vya mishahara ya Barca, lakini dalili zinaonesha kuwa mpango huo unaweza kukamilika kabla ya kuanza kwa michuano ya Euro.

# Pochettino alia na wachezaji Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amesema kikosi chake hakina ukomavu wa kushindana kila baada ya siku tatu kwenye Ligi Kuu England baada ya sare ya 2-2 na Sheffield United, Jumapili.

Chelsea, ambao waliilaza Manchester United mabao 4-3 wakiwa nyumbani Alhamisi iliyopita, walitangulia kufunga kwenye Uwanja wa Bramall Lane kupitia Thiago Silva, lakini wakarudishwa nyuma wakati Jayden Bogle alipofunga kabla ya kipindi cha mapumziko.

Noni Madueke alirejesha uongozi wa Chelsea dakika ya 66 kabla ya mshambuliaji wa Ollie McBurnie kusawazisha dakika za lala salama. Na Pochettino alisema ratiba ilivyo inawaweka kwenye wakati mgumu.

"Ni kweli, walikuwa wamechoka, lakini hiyo si kisingizio cha kutoshinda mchezo mwishoni," alisema Pochettino.

"Kutazama mpira wa miguu, ukiwa na umri wa miaka 52, unatambua haraka sana wakati timu iko tayari kushindana au la.

"Labda kwa sababu kundi hili bado halijakomaa vya kutosha kushindana kila mchezo, kila baada ya siku tatu, lakini tunapaswa kufikiria kidogo."

Pochettino pia alisema alimtoa mfungaji bora Cole Palmer katika dakika ya 74 kama tahadhari.

"Tunahitaji kumlinda," alisema.

"Tulitaka kumpa mapumziko na kujaribu kuzuia matatizo fulani katika siku zijazo."

Chelsea, ambayo iko katika nafasi ya tisa, itawakaribisha Everton katika ligi hiyo kabla ya kucheza na Manchester City katika nusu fainali ya Kombe la FA mnamo Aprili 20, mwaka huu.



## HABARI MICHEZO

# Gamondi aionya Yanga

INATOKA UKURASA 24

kucheza robo fainali na baadaye nusa na kisha fainali.

Gamondi alisema licha ya kuwakosa baadhi ya wachezaji kutokana na sababu mbalimbali, lakini anaimani na wachezaji waliopo fiti kwa mchezo huo kwenda kupambana na kupata matokeo mazuri mbele ya wapinzani wao hao.

Yanga itashuka dimbani kesho ikitoka kupoteza kwa mikwaju ya penalti 3-2 dhidi ya Mamelodi Sundowns kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa nchi Afrika Kusini Ijumaa iliyopita.

Mechi hiyo ilifikia changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya matokeo ya suluhu kwa dakika zote 90 za nyumbani na ugenini.

# Mo, Benchikha kujifungia

INATOKA UKURASA 24

Timu yoyote itakayoshinda itatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa wake huiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kocha Mkuu wa Simba, Benchikha amesema wanakwenda kucheza mechi hiyo muda mfupi tu baada ya kutoka mechi yao dhidi ya Al Ahly tena wakiwa ugenini, hivyo anatarajia kutakuwa na uchovu kwa wachezaji wake, lakini hiyo haiwezi kuwa kisingizio cha kutofanya vizuri kwenye mchezo wa leo.

"Tuna baadhi ya wachezaji ambao hawakucheza mechi ile tutawatumia, lakini pia wapo waliocheza ila watatumika kwa dakika kadhaa au zote kutegemea na mwenendo wa mechi," alisema

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah 'Bares', amesema kutokana na mazoezi ambayo amewafanyisha vijana wake, anaamini watafanya vizuri katika mechi ya leo.

"Tumekaa muda mrefu bila kucheza mechi yoyote, nadhani mara ya mwisho tulicheza dhidi ya hawa hawa Simba, Dar es Salaam katika mchezo wa Ligi Kuu, tuliwapa mapumziko mafupi wachezaji wetu, lakini walirejea na kufanya mazoezi ya nguvu kujiandaa na mchezo huu, naamini tutafanya vizuri," alisema kocha huyo.

# AZAM YAUTAKA UBINGWA FA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Azam FC ikisema inalitaka kwa udi na uvumba Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), maarufu kama FA Cup, Mtibwa Sugar imesema haina haja nalo kwani malengo yao ni kupambana ili kubaki Ligi Kuu.

Akizungumza juzi baada ya mechi ya hatua ya 16-bora dhidi ya Azam FC, nahodha wa Mtibwa Sugar, Oscar Masai, alisema hawakuutilia maanani sana mchezo huo kwa sababu akili yao ipo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayofuata dhidi ya Geita Gold utakaochezwa kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Aprili 13, mwaka huu.

**Katika mechi hiyo ambayo Mtibwa ilibamizwa mabao 3-0, beki huyo wa kati alisema kocha wao, Zuberi Katwila aliwaambia wakacheze kwa kufurahia soka na wasikamie sana kwa sababu wanaweza kutengeneza majeruha na kuwa hatari kwa mchezo ujao.**

"Tumeanza kufungwa bao la mapema, hatukuwa tayari, tulianza chini sana, wao wakatumia nafasi hiyo kupata bao.

"Mechi hii ilikuwa ni maandalizi ya mchezo unaofuata wa Ligi Kuu kwa sababu huko ndiko tunakoangalia sana, tunapambana ili tusishuke daraja.

"Mwalimu wetu alisema tuje kucheza mechi lakini 'tuinjoi' tu 'tusitoe macho' sana na wachezaji tukapata majeraha kwa sababu malengo yetu makubwa ni kwenye Ligi Kuu," alisema Masai.

Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema wachezaji wake hawakucheza vema katika mchezo huo badala yake kila mmoja alicheza kibinafsi.

"Pamoja na kushinda, lakini timu haikuwa vizuri, ni kawaida wakati mwingine kwa michezo ya aina hii," alisema kocha huyo.

Naye mmoja wa wafungaji wa bao moja kati ya hayo matatu yaliyowapeleka Azam hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, Abdul Selemani Sopu, alisema malengo yao ni kutwaa ubingwa na si kitu kingine chochote.

"Tulijua kuwa hii si ligi, hili ni Kombe la FA ukifungwa tu umetolewa, ni mechi inayohitaji ushindi tu, na hicho ndicho tulichojiandaa nacho, ndiyo maana tulianza kwa kasi kubwa lengo ni kupata bao la mapema na kweli ikawa hivyo. Malengo yetu ni kuchukua ubingwa huu wa Kombe la FA," alisema Sopu. Mabao mengine ya Azam yalifungwa na Feisal salum, Ayoub Lyanga.



Wafungaji wa mabao ya Azam FC dhidi ya Mtibwa Sugar, Abdul Selemani Sopu (kulia) na Feisal Salum 'Fei Toto', wakimpongeza Ayoub Lyanga (kushoto), kwa kuifungia timu yao bao la pili kwenye mechi ya CRDB Federation Cup, iliyopigwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Magnet Youth Sports yainunua Malimao FC*

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaendeleza soka hapa nchini uongozi wa Kituo cha Kukuza Vipaji vya Soka Tanzania, Magnet Youth Sports Academy, umeinunua timu ya Malimao FC ya Katavi, inayoshiriki Ligi Daraja la Pili Tanzania, imeelezwa.

Malimao FC iliyopo Katavi imewahi kucheza raundi ya pili ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini, maarufu FA Cup, na kutolewa na Azam FC kwa idadi ya mabao 9-0, mchezo uliochezwa Desemba 9, mwaka juzi.

Akizungumza na Nipashe jana katika uzinduzi wa kutimiza miaka 10 ya kituo hicho, Mwenyekiti wa Magnet, Tuntufye Mwambusi, alisema licha ya uwapo wa kituo hicho, lakini wamenunua timu ya Malimao FC ili kuendeleza soka la vijana.

Alisema baada ya kufanikiwa kununua timu hiyo ambayo sasa makazi yao yatakuwa Dar es Salaam badala ya Katavi, lengo kubwa ni kuwapa nafasi vijana wa kituo chao kupata nafasi ya kucheza katika ligi ya ushindani.

"Mbali na timu hiyo, mwaka huu mipango yetu ni kuboresha zaidi Ligi ya Inter Magnet, kufungua matawi mengine mawaili ya Magnet, kujenga uwezo na vikao vya kazi vya washiriki wetu kama Celta Vigo cha Hispania kwa vipindi bora vya mafunzo.

"Kutoa fursa zaidi na jukwaa kwa vijana katika ngazi za ndani na kimataifa, wahitimu wa kidato cha nne kuwa na programu ya mpira wa miguu na ujuzi, lakini pia kuunganisha wachezaji wetu wachanga na soka la Marekani kupata nafasi ya kujifunza mambo mbali ya soka," alisema Mwambusi

Aliongeza kuwa ndani ya miaka 10 ya kituo hicho wamefanikiwa kufungua vituo 10, nane vipo Dar es Salaam na Arusha viwili, huku pia wakifanikiwa kuanzisha ligi yao ambayo wachezaji wao wanaonyesha ujuzi wa soka na kupata nafasi ya kwenda kujiunga na washirika wao katika Kituo cha Celta Vigo, kilichopo Hispania.

Naye Mkurugenzi wa Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Salum Madadi, alisena anawapongeza Magnet kwa juhudu wanazozifanya katika kukuza vipaji vya mpira wa miguu ambavyo vitasaidia sana katika ngazi mbalimbali.

"Tumesikia vijana wameenda nje ya nchi, huko watakaporejea hawatarudi mikono mitupu bali watakuwa msaada mkubwa wa taifa letu, ikiwamo kupata nafasi katika timu zetu za vijana, hii linatakiwa kuigwa na vituo vingine," alisema Madadi.

Michezo
Nipashe
Jumanne Aprili 9, 2024



Pochettino alia na wachezaji UKURASA 22

BINJUKA...



Kiungo wa Manchester United, Carlos Casemiro, akijarubu 'kubinjuka' na mpira dhidi ya kiungo wa Liverpool, Alexis Mac Allister, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# MO, BENCHIKHA KUJIFUNGIA SIMBA

## Kumpa rungu la kusaka nyota wapya wa kimataifa, hasira CAF kwa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuishuhudia timu ya Simba ikishindwa kufikia malengo yake ya kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, amesema mwishoni mwa msimu atakutana na Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, kwa ajili ya kufanya tathimini ya kina na kukifanyia maboresho makubwa kikosi hicho.

**Simba wametupwa nje katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, kwa jumla ya mabao 3-0 katika michezo yote miwili nyumbani ikiruhusu bao 1-0 na kisha ugenini nchini Misri, kukubali kichapo cha mabao 2-0.**

Hata hivyo, jana Mo Dewji alisema ameziangalia mechi zote na ameona jinsi gani wachezaji walivyopambana na anaimani na utendaji kazi mzuri wa benchi la ufundi , hivyo anatarajia kukutana na kocha kwa ajili ya kuangalia mapungufu ya timu yao na kufanya maboresho.

Alisema watafanya maboresho kulingana na mahitaji ya kocha Benchikha, kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa kuleta wachezaji wenye uzoefu mkubwa wa kuwatoa hatua waliyofikia na kusonga mbele katika michuano ya kimataifa.

"Naipenda Simba sana, inapofanya vibaya naumia, tumefanikiwa kucheza robo fainali mara nyingi, tutafanya mabadiliko mwishoni mwa msimu huu kuboresha kikosi chetu kwa kuleta wachezaji wenye uzoefu kwa kuzingatia mapendekezo ya benchi la ufundi," alisema Mo Dewji.

Aliongeza kuwa matarajio yake makubwa ni kufanya maboresho kwa msimu ujao ili waweze kufikia malengo yao, akiamini kuwa hatua ya kufika nusu fainali itakuwa taratibu kama ilivyo kwa hapo awali kwani hakuna mtu ambaye anaamini Simba ingecheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika hatua nyingine, Simba leo itashuka katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma kuvaana na Mashujaa FC, kwenye mechi ya 16-bora ya CRDB Federation Cup.

Simba itashuka uwanjani ikiwa na kazi ya kutaka kuwafariji wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao wanaonekana kuhuzunika kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Al Ahly ya Misri kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, katika mechi iliyochezwa Ijumaa iliyopita Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, ikisukumwa nje kwa jumla ya mabao 3-0, kutokana na kufungwa bao 1-0 nyumbani.

Kutokana na kuondolewa kwa michuano hiyo, Simba imebakisha mataji mawili ambayo inaendea kupambana nayo kwa ajili kuyatia kibindoni nayo ni kombe hilo pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara, huku ikiwa tayari ina Ngao ya Jamii mkononi iliyoitwaa Agosti 13, ilipowachapa watani zao wa jadi, Yanga kwa mikwaju ya penalti 3-1, mechi iliyochezwa Agosti 13, mwaka jana, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Simba inakwenda kucheza na timu ambayo mara mwisho ndiyo iliyokutana nayo katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Machi 15, na kushinda mabao 2-0.

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi aionya Yanga FA Cup kwa Dodoma Jiji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema watakuwa makini katika mchezo wao wa hatua ya 16-bora wa Kombe la CRBD Bank dhidi ya Dodoma Jiji FC, kwani ni timu iliyowasumbua kwenye mechi ya Ligi Kuu, huku akihofia wachezaji wake kubweteka baada ya kutoka kucheza michuano mikubwa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kikosi cha Yanga kimeondoka jana jioni kuelekea Dodoma kwa ajili ya mchezo huo utakaochezwa kesho kwenye dimba la Jamhuri, jijini humo.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema wamejipanga vizuri kulingana na mchezo huo kuwa mgumu kwani mashindano hayo ni mtoano na anayefungwa anatoka.

Alisema walipata muda mfupi wa kufanya mazoezi kwa sababu ya kutoka katika mashindano makubwa na anatambua Dodoma Jiji FC mara ya mwisho iliwasumbua.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Dodoma Jiji FC ni wazuri na tuliwahi kucheza nao nyumbani na walitusumbua, mchezo huu tunatakiwa kuwa makini na kucheza kwa tahadhari kubwa ili kufuzu kucheza robo fainali," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa wanahitaji kutetea mataji yao yote msimu huu na ili kufanikisha malengo yao ni kushinda mchezo wao dhidi ya Dodoma Jiji FC na kwenda



INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >